Kuelezewa Kwa Uungu

Asante, Ndugu Carlson. Na salamu kwenu nyote ndugu na dada katika Bwana. Ni. . .Wakati mwingine hujisikia tu kidogo sitaki kusimama, wakati ninaposikiliza shuhuda nzuri kama hizo, na kadhalika, kama nilivyokuwa nikifanya asubuhi hii. Na, halafu, mwenyeji mwezangu katika taabu na mateso, kama ndugu yetu Mbatisti na dada waliyopitia; nikiwa hapo awali M—Mbatisti, mimi mwenyewe, Mmishenari wa Kibatisti, na—na nikijua vile inavyomaanisha wakati watu wako . . .

2 Nilikuwa na jambo lile lile. Watu wangu mwenyewe walinifukuza, nao walifikiri wangenifukuza kwa sababu nilikuwa nimeingia kichaa. Nami nika'gundua, na kwa kawaida nimelisema kidogo kwa namna fulani kwa njia isiyo dhahiri, "Kama mimi nina kichaa, hebu niacheni tu, kwa sababu nina furaha namna hii kuliko nilivyokuwa nilipokuwa na akili timamu." . . .Kwa hiyo hiyo kwa namna fulani ni falsafa yangu ndogo ninayoshikilia, yangu mwenyewe. Na—na bila shaka nimekuwa nikifurahia wakati huu—huu wa kuwa namna hii.

3 Na maskini ndugu huyu wa Kanisa la Kristo hapa, kama tunavyoliita kwa kawaida, la Kampbeli. Nami nakumbuka wao walikuwa wakiipinga vikali sana ile mikutano wakati wa mwanzoni tulipoanza. Lakini, mwajua, tulikuwa na mmoja aliyeitwa Paulo wakati mmoja alyekuwa wa namna ile ile, naye akawa mmoja wetu. Kwa hiyo nafikiri yale wanayoangalia kwa kawaida ni maisha unayoishi. Mwajua, ni afadhali uniishie mimi mahubiri kuliko kunihubiria mahubiri, wakati wo wote.

4 Wakati fulani uliopita, mhudumu mashuhuri, mtu mzuri wa Injili yote; yo—nyote mnamjua, nakisia. Ni Kasisi Booth-Clibborn; huhubiri Injili kwa lugha saba mbalimbali. Ana akili sana. Nami. . .Yeye ni jitu la akili. Basi tulikuwa tukitembea pamoja wakati mmoja, yeye na Ndugu Moore pamoja na mimi, nasi tulikuwa tunazungumza juu ya jambo fulani. Nami nilikuwa ninashikilia upande wa upinzani, ndipo akageuka akanitazama. Akasema, "Hujui tu Biblia yako." Mnajua jinsi Ndugu Booth anavyoweza kusema jambo hilo.

5 Nikasema, "Hiyo ni kweli, Ndugu Booth, bali ninamjua Mwandishi wake vizuri sana." Kwa hiyo, kwa hiyo mimi—mimi nataka . . .Mwajua, si kujua Neno Lake ni Uzima, bali, "kumjua Yeye ni Uzima." Hiyo ni kweli. Mnaona? Au najua neno Lake; kama ningemjua Yeye tu! Na hiyo bila shaka ndiyo Kweli.

6 Nilikuwa, asubuhi hii, nikipeana mikono na ushirika huu mzuri hapa, wa wahudumu. Hapa alikuwa ameketi huyu. . . sitaki kumfanya mtu ye yote aonekane mashuhuri. Lakini mtu

huyu mweusi aliingia, ndugu, akaketi pale. Nami nikamwambia katibu wangu hapa, “Yuko pale Mkristo halisi.”

7 Ananikumbusha sana juu ya Mzee Smith aliyekuwa wa Kanisa la Mungu katika Kristo, naamini. Nilikuwa nikiwahubiria sana kule chini, nami—nami ningali ninaweza kumwona bado. Yeye alifanana na ndugu huyu hapa, ila alikuwa kwa namna fulani na masharubu ya kijivu. Ningeingia kwa mlango wa nyuma, nami nisingesahau kamwe tamshi huyu mzee alikuwa akitoa; aliangalia juu, na watakatifu wote wangekuwa wanaimba, mwajua. Na kulikuwa na msichana mdogo aliyekuwa anakaa pembeni. Wimbo nilioupenda sana ulikuwa *Mwinueni Juu*. Nao wote wangepiga makofi, mtindo wa kipentekoste, mwajua, *Mwinueni Juu*. Wao walinipenda, nami niliwapenda. Na wakati tulipoingia . . . Yeye alizoea kuketi pale, huku ameweka kichwa chake *hivi*, kwenye dawati, na kuwaangalia tu, mwajua. Angesema, “Karibu, mzee. Pumzisha kofia yako. Pumzisha kofia yako.”

8 Ndugu huyu hapa; nilikuta kwamba, wakati huo, mmoja wa waimbaji wangu wa nyimbo za Injili niwapendao ni mke wake. Nami nikamshawishi sana nilivyoweza, kumfanya aimbe. Kisha, basi, akaomba asiitwe, nami najua jambo hilo lina maana gani. Bali nitamwalika mimi binafsi, kama anaweza, aje huku aimbe.

9 Hivi wewe siye yule dada aliyeimba—aliyeimba ule unaoitwa, *Meli Hoyee*, asubuhi moja kule kwa Wafanyi Biashara Wakristo, sasa? [Dada anasema, “Naam, bwana. Naam.”—Mh.] Natumaini mke wangu atapata nafuu juma hili, nami nataka akusikie, kwa sababu nimekusifu sana. Na kama ukikosa kuunasa huo kwenye kanda, tutalitatua jambo hilo. Napenda huko kuimba kuzuri.

10 Basi, nilizoea kuwaambia watu, mi—mimi nisingeweza kuimba. Loo, jamani, nilikuwa umbali wa maili milioni moja kutoka huko. Bali nikasema, “Kama ukipata kwenda Mbinguni na uishi kwenye jumba lako kuu la kifalme, wajua, kule Juu,” nikasema, “huko chini kabisa ya kilima, huko nyuma mwituni, nyuma kule, kuna kibanda kidogo kilichoko kule. Hicho kitakuwa ni changu. Basi moja ya asubuhi hizi utakapotembea kwenye ukumbi kisha umsikie mtu fulani amesimama kule juu, akiimba, ‘Neema Ya Ajabu! ni tamu jinsi gani, iliyookoa mwovu kama mimi!’ Sema, ‘Mungu asifiwe! Mzee Ndugu Branhama hatimaye alifaulu.’” Huyo atakuwa ni mimi huko juu, nikijaribu kuimba.”

11 Kwa ndugu zangu Wakristo na kwa . . . Naamini ndugu mmoja alimtambulisha yeye kwetu, asubuhi ya leo, kama mhudumu wa Kibudha, huku. Nakusalimu, ndugu yangu wa thamani. Nami nimekuwa na uhusiano mwingi, si mwingi kupita kiasi, lakini na watu wa Buddha; na hasa sana huko Canada,

miongoni mwa Wachina, nami nikawakuta ni watu wanaopenda watu sana na ni wazuri.

12 Namkumbuka maskini mtu wa Kibudha kutoka kwenye hekalu la Kibudha, alihudhuria mkutano wa Winnipeg, naye alikuwa ni kipofu. Ni watu wadogo sana, na wazuri sana, na bila shaka waliamini ya kwamba Mungu ni mponya. Basi nilipokuwa nikimwombea, naye alikuwa akirudiarudia, jinsi alivyompenda Mungu, mara macho yake yakafunguka, katika . . . Nalo lilikuwa jambo—jambo la ajabu sana. Kwa hiyo, tu—tunamthamini kila mwanamume na kila mtu.

13 Naam, sijakuwa na nafasi hii hapo awali, Chicago, kujaribu kuzungumza . . . Ambapo, nisingejaribu kuleta ujumbe fulani wo wote, kwa maana wahudumu hapa wanajiweza zaidi sana kuliko mimi, kuleta ujumbe. Bali, hata hivyo, hamko hapa kusikia ujumbe. Lakini nilifikiri kwamba ungekuwa ni wakati mzuri sana ambapo ningeweza kukutana na wahudumu wa Chicago, wilaya hii hapa, na kufahamiana zaidi nao, nasi tupate kujuana zaidi mmoja kwa mwingine. Nami bila shaka namshukuru Bwana kwa nafasi hii. Kwa sababu, nimekuja kwenye mji huu mara nyingi hapa, chini ya udhamini wa kanisa moja, na chini ya udhamini wa Wafanyi Biashara Wakristo; kwa hiyo, bila kupata nafasi ya kujieleza mwenyewe kwa ushirika wa ndugu.

14 Kisha—kisha nilifikiri, na kuna mambo mengi sana ambayo daima hufuata huduma kama hii, ya kuingia na kutoka, na heri na shari, mpaka wakati mwingine ni rahisi kwa mtu fulani kupata wazo baya. Nami nataka kuchukua dakika hizi chache zifuatazo kujaribu kueleza na—na kulifanya dhahiri kwa ndugu zangu, dhahiri nijuavyo namna ya kulifanya.

15 Nami—nami sistahili na siwezi kufanya ma—mazungumzo ambayo labda yangeonekana yana busara kwa watu wenye elimu. Sina elimu, nami nimekosa hiyo. Lakini nilikuwa . . . nampenda Bwana. Naye Bwana alinipa, labda, njia nyingine ya kuwaleta watu, kwa kipawa cha Kiungu, ambacho kingeweza kuziba mwanya wa yale wazazi wangu hawangeweza kunipa, elimu. Kutokana na nyumba ya jamaa maskini, na watoto kumi, na baba mgonjwa, nami sikupata nafasi ya kupata elimu. Kwa hiyo basi, lakini, wakati wa kuzaliwa, kuna jambo fulani lililotukia, tukio la Mungu, kwa mama na baba yangu. Nanyi mmeisoma hadithi yangu. Na, kwa njia hiyo, ninajaribu kuingiza sehemu yangu, pamoja nanyi ndugu, kuwavuta wenye dhambi kwa Kristo. Na sasa mimi . . .

16 Mimi si mshirikina. Lakini daima, kabla ya kulifungua Neno, napenda kuzungumza na Mwandishi wake kidogo. Basi na tuinamishe vichwa vyetu tena kwa muda kidogo.

17 Baba yetu wa thamani, Wewe ni Mungu wetu, nasi tunakukaribia Wewe kwa niaba ya Injili. Niko hapa mbele

ya watoto Wako, wachungaji Wako, na ndugu wa imani ile ile. Na jinsi inavyosisimua moyo wangu kuwasikia watu hawa ambao wameeleweka vibaya, na kupelekwa kwenye vituo vya uchunguzi, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu; kuona jinsi Wewe unavyowaita watoto Wako katika siku za mwisho.

18 Nasi kwa kweli kuamini, Baba, ya kwamba tunaishi katika mwisho wa mbio. Kama alivyosema nabii, "Kutakuwako na Nuru wakati wa jioni." Nasi tukiamini leo kwamba sisi ndio wajumbe wa Nuru hii kuu ya Injili ambayo, kwa neema Yako, Wewe umeturuhusu kuichukua hata miisho ya dunia, ambako ufufuo huu umeenda.

19 Basi naomba, Baba, ya kwamba, kutoka moyoni mwangu, ya kwamba Wewe utanijalia kuwaelezea ndugu zangu, asubuhi hii, kusudi na lengo la maisha yangu Kwako, ili kwamba wapate kufahamu. Jalia jambo hili, ya kwamba tupate upendo mkamilifu, na ushirika, na kushirikiana, katika matendo yote ya Injili. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu, Ambaye aliomba ya kwamba tupate kuwa mmoja kama vile Yeye na Baba Yake walivyokuwa Mmoja. Tukiamini jambo hili, ya kwamba, "Hili watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo, ninyi kwa ninyi." Amina.

20 Sasa hebu tu. . .Nami natumaini na kuamini ya kwamba siwachoshi ninyi ndugu na dada, juu ya jambo hili. Bali nafikiri ningetaka kujieleza dhahiri, ili kwamba isiwalazimu kusikia alilosema mtu mwingine. Na nimeeleza, mara nyingi, katika mikutano mingine ya wahudumu, lakini hii ndiyo mara yangu ya kwanza kwa kundi la Chicago, nami ningetaka kujijulisha vizuri sana, juu ya yale ninayojaribu kufanya.

21 Katika Injili ya kale iliyobarikiwa hapa, sura ya 26 ya Kitabu cha Matendo, tunasoma.

> *Kwa hiyo, Ee Mfalme Agripa, sikuyaasi yale maono ya mbinguni,*

22 Huyu anayezungumza, bila shaka, ni Paulo. Ambaye, sisi sote, kama wahudumu, tunapenda kurejea kwake, kwa maana yeye. . .Sisi, katika nia moja, tunaamini ya kwamba alikuwa mtume kwa kanisa la Kimataifa, ambaye Mungu alimwita awe sha—shahidi kwa Mataifa. Basi huduma yake ilikuwa imetiliwa swali.

23 Na kwa kawaida, jambo lo lote ambalo si la kawaida linapotukia, hudadisiwa. Ni, nami nafikiri ni sawa kabisa; linapaswa kutiliwa swali. Nami nafikiri ya kwamba wachungaji wakati mwingine wanashuku ma—mambo wanayosikia, nami nafikiri wana haki ya kushuku. Kwa maana, kama ninafahamu tafsiri ya jina *pasta*, inamaanisha "mchungaji." Na, kwa hiyo, yeye ni—ni—ni mlishi, ama mchungaji, wa kundi la wanaume na wanawake ambao Roho Mtakatifu amemfanya mwangalizi wake. Naye ana haki ya kujua ni chakula cha aina gani kondoo

wake wanapata, na mahali kinakotoka. Nafikiri ana haki ya jambo hilo.

24 Basi iwapo mchungaji, ama wakati mwingine watu, wangeonekana wakiwa kidogo wanashuku, jambo hilo, kamwe, halipaswi kumsumbua mtu ye yote. Linapaswa tu kuleta heshima kwenye moyo wa mtu, kwa mtu wa huo—huo msimamo, ambaye angetilia swali jambo hilo. Na, hata hivyo, kama huna hakika ya kwamba uko sawa, unawezaje kuenenda kwa imani?

25 Kama ukikusudia akilini mwako. . .Naam, hii inaonekana kama ni saikolojia; na huenda ikawa ndivyo ilivyo, na ndivyo ilivyo, bali ni sawa. Bali wewe kweli, kutoka moyoni mwako, ungefikiri usingeweza kuinuka kutoka mezani, labda usingeweza. Mnaona? Huna budi . . . Ni rahisi tu namna hiyo.

26 Huna budi kuamini. Huna budi kuwa na imani. Huna budi kuwa na ujasiri. Nawe unawezaje kuwa na ujasiri katika jambo lo lote ambalo—ambalo hata hujui unakoelekea? Ningewezaje kusafiri kwenye njia ambayo sijawahi kusafiri hapo awali, katika mwendo wa kasi sana, na kila mahali kwenye kona, bila kujua kona inayofuata ina nini? Huna budi kuona unakoelekea, la sivyo hujui jinsi ya kutembea. Na hivyo ndivyo kila mmoja anapaswa kuwa. Ndipo unapoweza, unaliona, linafunuliwa kwako, nawe unajua unakoelekea, basi hakuna kitu kitakachokuzuia.

27 Na hivyo ndivyo, ninavyofikiri, Paulo, alivyokuwa anajaribu kumwambia Agripa hapa. Ya kwamba, a—aliwaambia ya kwamba, "Wakati mmoja nilikuwa mmoja wenu."

28 Nami nadhani, labda, kama—kama ndugu huyu wa Kibatisti, angeenda kwenye kanisa la Kibatisti asubuhi ya leo, yeye na mke wake, huo labda ungekuwa ndio ushuhuda wao. "Ni—nilikuwa mmoja wenu wakati mmoja."

29 Ama, Kanisa la Kristo, ama ndugu Mkampbeli hapa, angeenda kwa—kwa watu wake. Naamini linaitwa jina bora zaidi; Wanafunzi wa Kristo, ndivyo wanavyoliita, bali kweli ni fundisho la Alexander Campbell. Ndipo basi Kanisa la Kristo lilitoka kwenu, kwa sababu ya muziki. Hiyo ni kweli, sivyo? Na kama angaliweza kurudi kwao, yeye angesema, "Siku moja nilikuwa mmoja wenu."

30 Basi Paulo anarudi hapa kwa Mfalme Agripa, na Festo, akasema, "Siku moja nilikuwa mmoja wenu. Nilikuwa Mfarisayo wa Mafarisayo." Yeye alikuzwa chini ya Gamalieli, yule mwalimu mkuu, naye alijua amri zao zote na kanuni, na kile tu walichoamini na kile ambacho hawakuamini. Naye alisema, "Hata nililisaliti Kanisa la Mungu hata kufa." Mnaona? Akasema, "Jambo lile lile ninaloulizwa juu yake, nilikuwa mtesi wake."

31 Daima nimewaza ya kwamba kifo cha Stefano hakina budi kilimwingia Paulo, maana alipoona kule kuonekana kutukufu

kwenye uso wa Stefano. Alipoangalia juu, huku mabonge ya udongo yakimpiga hata kufa, yeye alisema, “Namwona Yesu akisimama upande wa mkono wa kuume wa Mungu.” Nanyi mwajua, unaweza kumwua mjumbe, bali huwezi kuuua Ujumbe wake. Huo ni Kweli. Na ujumbe huo, ingawa Stefano alikuwa ameaga dunia akaenda kukaa na Yesu, hata hivyo, ujumbe wake uliendelea, kwa maana Paulo aliendelea kuzungumza juu yake, na, kwamba, yeye ndiye “aliye mdogo sana” kati yao, wala hakustahili kuitwa mmoja, kwa sababu alikuwa ameshuhudia na—na kutoa kibali chake kumwondoa mtu huyu mtauwa.

32 Kwa hiyo, Paulo, kama vile watu wote, mbele ya watu, angepaswa kufanya, Paulo anachukua tukio la—lake, huko nyuma, tangu mwanzo, kwa kile alichokuwa; kisha analiweka, na kulitilia msingi kwenye Maandiko, kuonyesha ya kwamba kile alichokuwa anafanya kilikuwa cha kimaandiko. Ingawa ilikuwa ni kinyume cha imani yao, hata hivyo alikuwa akiwaonyesha ya kwamba lilikuwa ni Maandiko.

33 Kwa hiyo, nafikiri kwamba sisi. . .Cho chote, kama ninavyosema mara nyingi, ndugu zangu, ninyi ambao mmekuwa kwenye mikutano, ya kwamba, kama wakati wote nikikutwa nikinena mambo ambayo si ya kimaandiko, basi nafikiri ni kweli kwamba . . . ama ndugu mwingine ye yote, tunapaswa kukutana na kusema, “Hilo halipatikani katika Biblia,” mnaona. Kama liko kwenye Biblia, huenda ukawa na fasiri tofauti; lakini, ni, kama liko kwenye Maandiko, sawa.

34 Naam, Paulo alikuwa akitoa tafsiri yake ya yale nabii aliyosema, na yale Musa aliyosema, yakija kutimia. Ndipo akakutana na Yesu njiani, katika ono. Ndipo huyu Yesu akamwita.

35 Jambo ambalo, lisingekuwa jambo gumu kwa hao Wayahudi, kama alivyosema, “Ee mheshimiwa Festo,” na—na kadhalika, kwamba “lingekuwa jambo geni kwako, kwamba Mungu angewafufua wafu?” Mnaona? “Kwa maana kama unajua kile Mungu alichokuwa kule nyuma, kwa Ma—Maandiko, kweli ungejua ya kwamba Yeye anaweza kuwafufua wafu.”

36 Kisha akasema, alikuwa amewapa lile tukio la kule njiani akienda zake Dameski, juu ya kile kilichotukia, kwamba, kuwaacha wajue ya kwamba huyu Yesu ambaye—ambaye walikuwa wakisababisha vurugu nyingi sana juu yake wakihubiri Hilo, alikuwa Mungu yeye yule waliyekuwa wamemtumikia wakati wote. Kwa maana, alikuwa nyikani pamoja nao, Ambaye aliwaongoza, akiwa Nuru ile; ule Moto, Nguzo Ya Moto iliyowaongoza. Naye akamtokea Paulo katika kitu kile kile, ile Nuru tena, ambayo ilimpofusha. Ndipo akauliza, “U nani Wewe, Bwana?”

37 Ndipo akasema, “Mimi ni Yesu, ambaye unaniudhi. Na ni vigumu kuipiga teke michokoo.”

38 Basi alikuwa akijaribu kuwaeleza ilikuwa ni nini, na—na alikuwa akijaribu kuwafundisha ya kwamba, jambo alilokuwa akiwaonyesha watu, jambo hilo lilikuwa, ya kwamba, "Yesu Kristo alikuwa Masihi, na ya kwamba Yeye alikufa, na Mungu alimfufua." Na jambo hilo lilikuwa ni kulingana na Maandiko. "Na ya kwamba sasa alikwisha paa Juu, kwa Mungu Baba," ya kwamba—kwamba yeye alikuwa shahidi wa ufufuo Wake. Na ya kwamba, miujiza hii, na ishara, na maajabu, ambavyo vilikuwa vigeni mbele za watu, havikuwa vitu vigeni kwa mwamini halisi wa Kimaandiko, kwa maana Biblia ilikuwa imenena habari hizo.

39 Angalia huko nyuma katika manabii, jinsi lilivyotabiri, habari, juu ya kuja kwa Masihi, na yale angefanya. "Viwete wangeruka kama ayala," katika Isaya 35 na Maandiko mbalimbali ambayo angeyarejea. Hatujayaandika hapa, lakini labda kurudi nyuma na kuyarejea katika hutuba yake fupi mbele za wale wafalme; kwa maana, labda wasingekuwa na subira Naye kama mlivyo nayo kwangu. Kwa hiyo, halafu a—alikuwa akilielezea jambo hilo, na kujaribu kuwaambia ya kwamba Mungu yeye yule waliyemtumikia . . .

40 Halafu, tena, akasema, "Kwa njia ile ambayo waiita *uzushi*," hiyo ni kusema, "kichaa," mnaona. "Njia waiitayo uzushi, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu mnayemwamini." Mnaona, "Kwa njia waiitayo uzushi."

41 Nina hakika ya kwamba, leo, kama tungelisimama na makanisa ya hapo awali ambayo tulikuwa wafuasi wake, kama vile Presbiteri, Katoliki, Batisti, na mengine mbalimbali, tungetoa ushuhuda ule ule kwa watu hao, ambao wanasema ya kwamba wanataka, kama, kumweka ndugu katika hospitali ya wenda wazimu, ama kitu kama hicho. "Kwa njia ambayo wanaiita uzushi, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa Baba zetu."

42 Basi ni ushuhuda mzuri namna gani ambao ulikuwa mbele ya Agripa, na hata katikakati ya mazungumzo yake, Agripa akapasa sauti kuu, akasema, "Paulo, Sauli, karibu umenishawishi kuwa Mkristo." Mnaona, jinsi, aliyvoyaleta Maandiko dhahiri sana, ingawaje ilikuwa kinyume cha sinagogi lake. Bali Maandiko yalikuwa dhahiri sana, hata akasema, "Wewe karibu unishwawishi kuwa kama ulivyo wewe."

43 Paulo akasema, "Ningetaka ungalikuwa, kwa jumla, ila nisingetaka wewe uwe katika minyororo hii niliyo nayo mimi, mnaona," bali kuwa mwamini kama alivyokuwa yeye. Kwa maneno mengine, kama mimi . . ."Naomba Mungu kwamba utaona ufunuo kama—kama ninavyouona." Kwa maneno mengine, "Ningependa ungalifanya hivyo." Mnaona? "Ningetaka tu ungaliweza."

44 Wakati, Festo, naamini, alikuwa amemwambia ya kwamba alikuwa "amesoma sana," alikuwa "ameingia kichaa." Bali akamjulisha ya kwamba ha—hakuwa hivyo; ya kwamba yeye a—alijua alipokuwa.

45 Nami ningesema hivi, asubuhi ya leo, ndugu. Kwa jumla ninataka kama ninge-. . .si kumaanisha maisha ya Paulo, bali ni kusudi tu nitoe matamshi madogo ya kimsingi. Kwa maana, kuna wengi zaidi hapa ambao labda watazungumza asubuhi ya leo, bali nilitaka nafasi hii kusema jambo hili. Sasa ningetaka kila kanisa lingine, kama nilivyowasikia mkishuka mkienda, Hekalu la Betheli, Indipendent, Assemblies of God, na mengine mbalimbali. . . Ningetaka kwa jumla mngeweza kuona kile ninachoona; kwamba mngeweza. Ningetaka mngaliona ono ninaloona, ndipo mngekuwa na ufahamu wa dhahiri zaidi, wa huduma hii.

46 Nilipoliacha kanisa la Batisti kuingia katika Pentekoste; basi Dk. Roy E. Davis, aliyekuwa ameniwekea mikono katika Kanisa la Mishenari la Kibatisti, aliniambia ya kwamba nilikuwa na jinamizi, wakati ono la Bwana lilipokuja na—na kunena nami. Nanyi—nanyi mnajua kuponya kulikuwa nini wakati huo, kulikuwa duni.

47 Na—nami sikujua kitu juu ya Wapentekoste. Nilisikia walikuwa kundi la watakatifu wanaojifingirisha waliolala sakafuni wakitokwa mate kama mbwa wenye kichaa, nao iliwabidi kuwapepea hewa wapate kujirudia, na mambo kama hayo. Hayo tu ndiyo niliyojua juu ya Wapentekoste.

Akasema, "Unafikiri ni nani atakayekusikiliza?"

48 Nikasema, "Kama Mungu ananituma, kuna mahali fulani na mtu fulani anayenituma kwake." Hiyo ni kweli. Mnaona? Kwa sababu, nilisema, "Dk. Davis," nikasema, "Yeye alikuwa halisi tu; Nilisimama na kumtazama Yeye," nikasema. Wao waliniambia ya kwamba maono hayo. . .

49 Mimi ni mwamini mkuu, ndugu, ya kwamba— ya kwamba karama na miito havina majuto. Ni—ninaamini jambo hilo. Unazaliwa, huwezi kuwa kitu usicho. Na kila unapojaribu kujifanya kitu fulani usicho, unatekeleza tu sehemu ya mnafiki. Na Mungu anijalie nife kabla sijakuwa mnafiki, mnaona. Hebu niwe tu vile nilivyo, halafu nilifanye dhahiri na wazi. Halafu—halafu, basi, hebu—hebu niwe hivyo, halafu kila mtu anajua. Ndipo unajua tu hasa.

50 Na kwa hiyo sasa, kama mjuavyo, sikupata kusoma sana, kama nilivyosema. Kwa hiyo nini hii yangu. . .katika theolojia, mimi ndiye mtu duni kabisa aliyeko. Nami nafikiri mnajua jambo hilo, mnaona. Pia kama mhubiri, ingekuwa vigumu kwangu kujiita mmoja, kwa sababu ya kutopata masomo na kujua maneno, na kadhalika. Bali yale machache niliyo nayo, ku-,. . .kuhusu maarifa yangu ya kumjua, kwa neema Yake,

Bwana Yesu, mimi hujaribu kushiriki hayo pamoja na ndugu zangu wote kila mahali, kushiriki jambo hili.

51 Ndipo, lakini, nilipoliacha kanisa la Kibatisti; ambalo ndilo kanisa pekee nililowahi kuingia, ama nilimowekelewa mikono. Basi nilitawadhwa katika mwaka wa 1933, katika Kanisa Batisti la Kimishenari, Jeffersonville, Indiana. Ni m—m . . . mshirika wa Shirika la Batisti ya Kusini. Wakati huo sisi, katika wakati huu, mimi . . . nilipotoka na kunini hii tu . . .

52 Naam, kanisa la Kibatisti ni kanisa linalojitawala. Sote—sote tunajua jambo hilo, ya kwamba ni—ni . . . Unaweza kuhubiri karibu juu ya cho chote utakacho, iwapo kusanyiko lako litalivumilia. Wao wananini hii tu . . . Unataka kuhubiri cho chote utakacho.

53 Nami napenda jambo hilo, mnaona, kwa maana ninaamini ni la kimitume. Kwa kuwa, kiongozi, cheo kilicho cha juu sana kanisani, ni mchungaji, tunatambua jambo hilo, mchungaji. Na—na iwapo a—a- . . . Kama askofu fulani ama mtu mwingine ataondoa ufunuo kutoka kwa mchungaji, basi Mungu kamwe atatendaje kazi katika kanisa Lake? Mnaona, huwezi kuupata. Kwa hiyo nina . . .

54 Nilipokuja kule, nilikutana na kundi la kwanza, ambapo ilikuwa ni kule kuponywa kwa mtoto Betty Daughtery, kule St. Louis, Missouri. Na ilikuwa ni Pentecostal United, ama kanisa la Kipentekoste la Jina la Yesu, ambalo mchungaji huyu alikuwa mfuasi wake, ndipo msichana wake mdogo akaponywa. Kwa kweli, nilifikiri jambo hilo ndilo lililomfanya mpentekoste, ni kwa kuwa walijiita wenyewe, "Yesu Pekee." Basi nilifikiri jambo hilo ndilo lililowafanya wapentekoste, ni kwa sababu hivyo ndivyo walivyojiita wenyewe, na tofauti ilikuwa hiyo. Kwa hiyo, vema, basi kutoka hapo nikaenda kwa . . .

55 Na mtu mzuri; alikuwa na mkutano mkuu kule St. Louis, ambako ile picha inatokea. Tulikuwa tumekodi Ukumbi wa Kiel; na usiku wa kwanza, ama wa pili, kumi na nne elfu waliojazana mle, nasi hata tusinge- . . . ilitubidi kuwaweka polisi milangoni kuwakataza kuingia.

56 Halafu basi kutoka hapo, kushuka chini kwenda kwa Richard T. Reed, wa Maskani ya Blessed Old Bible Hour huko Jonesboro, ambalo lilikuwa la shirika lilo hilo pia. Na kutoka huko, tukaenda kwa Dk. G.H. Brown, shirika lile lile, kwenye Barabara ya 505 ya Victor huko Little Rock, Arkansas. Na, kutoka huko, tukaenda kwenye Pwani ya Magharibi.

57 Halafu nilipofika kwenye Pwani ya Magharibi, nikawasha moto. Ndipo nikakuta kwamba kulikuweko na migawanyiko mingi kati ya wapentekoste, katika madhehebu yao, kama tuliyo nayo sisi Wabatisti. Mnaona, wao walikuwa—walikuwa na tofauti nyingi sana, walizokuwa nazo, walitofautiana. Kulikuwako na Assemblies of God, na Church of God, na kitu

kingine, na kitu kingine, na kitu kingine, na—na kutofautiana. Nao walijitenganisha wenyewe, na walikuwa wameweka mipaka midogo. Ndipo ndugu wengine wote wakaanza kunijia, na kuniambia, "Mbona, wewe ni Yesu Pekee, pamoja na kundi hili hapa."

Nikasema, "La, si—sijiiti mwenyewe hivyo." Mnaona?

Yeye akasema, "Mbona, unashirikiana nao?"

58 Nikasema, "Vema, hilo—hilo halinifanyi kuwa hivyo." Mnaona. Kisha nikasema, "Ni—ni—nina nini hii tu . . . Wao walikuwa ni ndugu."

59 Naye akasema, "Mbona, wao ni kundi la . . . Mbona, hawana kitu ila kundi la viota vya nderi na kadhalika, kila mahali, namna hiyo. Ambapo . . . "

60 Nikasema, "Sasa, samahani. Ninakutana na watu watauwa kweli kule. Nao ni watu wa Mungu." Basi nikasema, "Bila shaka ina—inaniudhi kuwaita wao unapowaita waovu; kwa maana, si waovu."

61 Vema, ndipo nilijaribu kujizuia kadiri nilivyoweza, bila kuelezea upande wo wote. Vema, nikaanza kuchunguza mawazo yao yalikuwa nini, na matengano yao yalikuwa ni nini, na ni nini kiliwafanya watengane. Ndipo nikakuta kwamba mawili ya hayo makundi makubwa, moja lao liliitwa Yesu Pekee, na lile lingine liliitwa Assemblies of God. Nao walikuwa wametoka, ama kutengana, juu ya swali la ubatizo wa maji; moja likitumia "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," na hilo lingine likitumia Jina la "Yesu."

62 Vema, nikatazama, na pande zote mbili kulikuweko na watu wakuu, watumishi wa Mungu. Ndipo nikawaza, "Ee Mungu, laiti ningaliweza kuwaona wote wameungana, na wakaendelee tu mbele na kuwa . . . lakini wasiweke mipaka, na kusema, 'Hatutashirikiana mmoja kwa mwingine.'" Lakini nikaona kwamba, katika jambo hili, pepo mchafu alikuwa ameingia kati yao na alikuwa amesababisha chuki na kijicho, juu ya maswali yaliyozuka miongoni mwao. Nikawaza, "Jambo hilo ndilo hasa Ibilisi anataka. Hilo ndilo tu analotaka. Mradi tu mmelengana bunduki, haitambidi kutupa hata konde moja." Nami . . .

63 Kwa hiyo basi, hatimaye, likafikia kwenye shindano la kuamua. Na shindano hilo la kuamua lilikuwa kule Seattle, Washington, yapata mwaka wa 1946. Basi asubuhi moja nililetwa kwenye sebule ya hoteli, mahali kama hapa, tukiwa kwenye ki—kifunguakinywa cha baadhi ya wahudumu. Nami ilinibidi kuzungumza na wale watu wawili muhimu.

64 Mmoja wao alikuwa Dk. Ness. Nafikiri ninyi ndugu wa Assemblies of God mnamkumbuka. Alikuwa katika mkoa wa kaskazini-magharibi; mtu mashuhuri sana, mwerevu, mwanachuoni. Naye aliwawakilisha Assemblies of God.

65 Halafu, Dk. Scism, wa kanisa la United Pentekoste. Nafikiri ninyi ndugu wa United Pentekoste mnamkumbuka. Yeye pia alikuwa wa mkoa wa kule kaskazini-magharibi, ambako alikuwa kiongozi wao na wilaya za kule.

66 Vema, watu hawa wawili wakakutana. Nami nilikuwa niletwe mbele yao, kwa maana ma—makali yalizidi kuwa makali, na yalikuwa yakinikata kutoka kila upande. Basi nikafikiri, "Yanibidi nifanye nini? Ninaweza kufanya nini?"

67 Ndipo, Vema, wao wakasema, "Vema, huna budi kujiunga na moja ama lingine. Iwapo utaambatana na Jina la Yesu, huna budi kuwa wa Jina la Yesu. Na iwapo utaambatana na Assemblies of God, huna budi kutoka kwenye Jina la Yesu, uwe Assemblies of God, ama kadhalika." Ilifikia mahali ambapo ilinibidi kujitokeza kwa namna fulani.

68 Niliomba sana asubuhi hiyo kabla sijaenda kule. Nikasema, "Mungu, nisaidie. Kwa maana, kuna watu wawili wakuu; kuna maelfu ya watumishi. Nawe umenituma huku nje nikiwa na huduma. Nao wote wawili ni watumishi Wako. Basi je! nitumie ushawishi mdogo nilio nao kwa madhehebu moja wakati yanapigana na hayo mengine?" Mnaona? "Ni—nisingeweza kujisikia vema katika kufanya jambo hilo. Sidhani kwamba yangekuwa ni mapenzi ya Kristo kwangu kufanya jambo hilo." Ndipo nikasema, "Mungu, nisaidie na unipe jambo la kufanya, ama unipe jambo la kusema."

69 Basi sikuwa na mtu ye yote. Ilinibidi tu kusimama pale, mimi na Bwana Yesu tu asubuhi hiyo.

70 Vema, ule mjadala mkubwa ukaja. "Utafanya nini? U—u—utatoa uamuzi gani?"

71 Nikasema, "Uamuzi wangu tayari umefanywa. Kwamba, uamuzi wangu, ni kusimama katikati ya ninyi wawili, na nisijiunge na madhehebu yo yote; na kusema, huku nimewakumbatia nyote wawili kwa mikono, 'Sisi ni ndugu.'" Mnaona? Mnaona, sisi ni ndugu. Mnaona? Kisha nikasema, "Nimejaribu kusoma vitabu vyote niwezavyo, jinsi jambo hili lilivyozuka, lililoitwa 'swala jipya,' na jinsi walivyojitenga wenyewe, na jinsi ambavyo *hili* lilivyoanza namna hii na namna ile." Halafu nikasema, "Katika mabishano kati yenu," nikasema, "jambo lilo hilo ndilo lililouvunja mwenendo wa kipentekoste, kwenye siku. . . baada ya Pentekoste. Walianza kubishana wao kwa wao." Kisha nikasema, "Kitu hicho kinatenganisha tena."

72 Nikasema, "Je! kuna uwezekano ya kwamba kungekuwa na njia kati yenu, ndugu? Kuna kitu ambacho—ambacho kingeweza kusimama?"

73 Vema, wasingeweza kufungua mdomo wao juu ya jambo hilo, kwa sababu lilikuwa kali sana. Mnajua, yapata miaka kumi na mitano, ishirini iliyopita, kwa sababu kundi moja ndiyo kwanza lijitenge na hilo jingine, na kulikuwa na ugomvi mwingi.

74 Kwa hiyo nikasema, "Vema, ndugu, nitafanya jambo hili. Nita-. . . Mungu kamwe hakunituma kubatiza, hata hivyo. Yeye alinituma kuwaombea watoto Wake wagonjwa." Nikasema, "Kwa hiyo, nita—nitawaombea hao watoto wagonjwa, nanyi wahudumu fanyeni ubatizo wenu wenyewe," nikasema.

75 Nikasema, "Sasa ninataka kuwaulizeni jambo fulani, kusudi tu mpate kuelewa:" Nikasema, "Ndugu Ness, hawa watu wa Jina la Yesu, unaamini ya kwamba wamempokea Roho Mtakatifu wanaponena kwa lugha na kufanya mambo yale yale ambayo ninyi katika Assemblies of God mnafanya?"

Kasema, "Bila shaka."

76 Nikasema, "Ndugu Scism, unaamini ya kwamba Assemblies of God wana Roho Mtakatifu wanaponena kwa lugha na kufanya jambo lile lile mlilofanya mlipobatizwa?"

Akasema, "Bila shaka, naamini."

77 Nikasema, "Naam, Biblia ilisema, 'Mungu huwapa Roho Mtakatifu hao wanaomtii.' Basi, ni nani waliomtii? Ni nani waliomtii? Ni nani kati yenu aliyemtii? Na Mungu aliwapa nyote wawili Roho Mtakatifu, mnaona?"

78 Nikasema, "Hivi ungeweza kusema, Ndugu Scism, ya kwamba Ndugu Ness hana Roho Mtakatifu?"

Kasema, "La."

79 Nikasema, "Ungeweza kusema ya kwamba Ndugu Scism hana Roho Mtakatifu?"

80 "La." Mnaona? Ya kwamba, wote wawili waliamini kila mmoja wao alikuwa na Roho Mtakatifu.

81 Lakini, mnaona, haina maana kabisa, ndugu. Haina maana. Ndipo nilisikia, baadaye kidogo kutoka hapo . . .

Nitarudi kwenye jambo langu hivi punde.

82 Ndugu wa huko Finland, baada ya mimi kuondoka Finland; ambako Mungu alitupa, niliofikiri, mmoja wa mikutano yetu mikuu sana. Kule ambako yule mvulana mdogo aliyekufa alifufuliwa, na mambo mengi. Nilikutana huko Stockhom, Sweden, na Lewi Petrus wa kanisa la Filadelfia kule ambaye ni mtu mkuu wa Mungu, nalo kanisa la Filadelfia. Ndugu Gordon Lindsay, aliyekuwa sasa . . . nadhani. Sidhani yeye ni mfuasi wake sasa, bali alikuwa mfuasi wa Assemblies of God.

83 Na Assemblies of God ni moja la wadhamini wangu wakuu, kimataifa. Na Foursquare, ambalo lilikuwa limejitenga na Assemblies of God, ni moja la wadhamini wangu wakuu. Umoja, kimataifa, ni moja la wadhamini wangu wakuu. Mnaona? Nami nilichukua tu msimamo huo, nikiacha tu makali yaliyo kali, kisha nikachukua msimamo, ya kwamba sitaungana na upande wo wote wa mzozo huo. Mpaka tunapoweza kuona sisi ni ndugu, na kukutana pamoja, ndipo basi tuta—tutaona jambo

lilo hilo moja pale, ambalo tutafikia—kusudi na nia ya kufanya jambo hilo.

84 Basi hu—huna budi kuchunguza kusudi na nia yako, kwanza. Kwanza, tafuta kujua mapenzi ya Mungu; kisha tafuta kujua nia yako; halafu basi uchunguze kusudi lako uone kama kusudi lako ni sawa. Halafu, kama Yesu alivyosema katika Marko 11:24, "Kama ukiuambia mlima huu, 'ng'oka,' wala usione shaka moyoni mwako." Bali mradi tu una shaka moyoni mwako, kama ni mapenzi ya Mungu, ama kusudi ama nia yako ni mbaya, utang'okaje? Bali unapojua ya kwamba kusudi lako ni sahili, na ni mapenzi ya Mungu, na nia yako ni sahili, huo hauna budi kung'oka. Hivyo tu, la sivyo Mungu alisema jambo ambalo si kweli.

85 Hiyo ndiyo sababu hasa, ninapokwenda jukwaani, katika makanisa, hakuna mtu amewahi kunisikia nikitaja mambo hayo jukwaani, maswala hayo. Ninayaacha tu yalivyo. Mnaona, hiyo ni juu yenu enyi wanaume. Mnaona? Mimi niko hapa kuwasaidia kuwavuta watu kwa Kristo, kwa karama ya Kiungu, mnaona. Mnaona? Haileti tofauti yo yote. . . Ninyi batizeni. Lakini basi inapofikia. . .

86 Bila shaka, nimeitwa kila kitu. Nimeitwa, sijui vitu vingapi, po pote kutoka "mwana wa Mungu aliyefanyika mwili" mpaka "i—ibilisi." Hiyo ni kweli, kila kitu. Bali, nyuma ya hayo yote, mimi ndugu yenu, mwenyeji pamoja nanyi wa Ufalme wa Mungu; nikitenda kazi pamoja nanyi nyote, kwa ajili ya Ufalme. Na hiyo ni kweli.

87 Sasa mimi nitanini hii, kama ni sawa, na mnafikiri tuna wakati wa kutosha, ningetaka kuwaambia jinsi tulivyojadiliana jambo hilo. Lingekuwa jambo zuri, ndugu zangu, kwa muda kidogo tu? [Wahudumu wanasema, "Endelea. Hakika."—Mh.] Ndugu, Ndugu Ness na hao wengine. . . Vema. Na huenda ikawa ni kidogo ambayo yatawasaidia. Ingewasaidia kufahamu, kwa namna fulani.

88 Niliandika, hapa, baadhi ya mambo ambayo nilikumbuka. Niliyatoa pale. Basi waliniuliza, niliamini nini juu ya "utatu," Je! niliamini ya kwamba kuna "utatu" wa Mungu?

89 Sasa, enyi ndugu, tunapoliendea jambo hili, natumaini ya kwamba, wakati litakapokwisha, ya kwamba tutakuwa ndugu wale wale ambao tumekuwa wakati huu wote. Mnaona? Bali ninajisikia ya kwamba ninawawia, kwa kuwa watu wenu huja kwenye mikutano yangu, nami bila shaka nisingetaka kumwachilia hata mmoja wao aondoke, huku amedanganywa.

90 Na daima nimewaambia watu wanaoniandikia maswali, nje ya yale ninayohubiri jukwaani. . . Na huyu hapa katibu wangu, na kadhalika. Kama wao wakiniuliza swali, "Na jambo *hili* je? ama na *lile* je?"

91 Nikasema, "Mwulize mchungaji wako, mnaona. Kwa sababu, iwapo yeye amekuongoza umbali huu, hata ukampokea Roho Mtakatifu, atakuongoza mbele, mnaona. Wewe, unaona, mwulize mchungaji wako." Kwa maana, vitu vidogo kama hivyo husababisha mchafuko, na kwa hiyo, ninaliachilia mbali, mwaona.

92 Sasa, imesemwa ya kwamba nilikuwa m—mpiga vita madhehebu. Naam, siyapigi vita. Nafikiri ya kwamba madhehebu ni mazuri sana, bali wakati utaratibu wako wa kimadhehebu yako unapooza, jambo hilo ndilo ninalopinga. Mnaona? Haidhuru kama ni umoja, ama—ama ni utatu, ama yo yote yale, utaratibu; ambapo unapofikia mahali, wewe sasa . . . na kusema, "Sisi ni Assemblies of God!"

"Vema, ni nani yule upande wa pili wa barabara?"

93 "Loo, hao ni ndugu zetu. Wana—wanaitwa United Pentecostal."

"Vema, ni nani yule pale?"

94 "Loo, hao ni ndugu wa Foursquare. Loo, sisi ni ndugu wazuri sana. Tuna ushirika mzuri sana, mmoja kwa mwingine."

"Loo, hivi ninyi mnaamini jambo lile lile?"

"Loo, naam, tunaamini . . ."

"Vema, ni nini kinachokufanya namna hii?"

95 "Vema, *hawa* ndugu wanabatiza namna *hii*. Na *hawa* wanabatiza namna *hii*, kifudifudi. Na *hawa* wanabatiza . . ."

96 Kama vile huko Afrika Kusini kule, ndugu, tulikutana na jambo hilo. Wao waliniuliza. Kundi moja linabatiza mara tatu kifudifudi. Na hilo lingine linabatiza mara tatu, kichalichali. Nao wakasema . . . Nikasema, "Mlipata wapi jambo hilo?"

97 Mmoja akasema, "Wakati Yeye alipokufa, Biblia ilisema aliinama mbele," kisha kasema, "kwa hiyo inatupasa kuwainamisha mbele."

98 Ndipo nikasema, "Vema," kwa kundi hilo lingine, "vipi . . . Na ninyi je?"

Kasema, "Umewahi kumzika mtu kifudifudi?"

99 Vema, na wajua nini? Wao walijitenga wakafanya makundi mawili, madhehebu mawili. Loo, rehema, ndugu! Hilo ndilo tu Ibilisi alalotaka. Hilo ndilo tu analotaka. Naam. Jifanyeni . . .

100 Naam, mnaona si Misheni ya Imani ya Kimitume, ama—ama wala—wala si Pentecostal Assemblies, upande ule mwingine. Si hayo. Kuna watu wazuri katika makundi yote mawili, kama ilivyo hapa. Lakini, mnaona, ni utaratibu wa kitu hicho.

101 Ni kama tu Katoliki, kama ninavyosema mara nyingi. Kama yeye ni Mkatoliki, na anamtegemea Kristo kwa ajili ya wokovu wake, yeye ameokolewa. Bila shaka, hiyo ni

kweli. Iwapo anategemea kanisa, amepotea. Na ye yote wenu ndugu wa kipentekoste anajua, kama tunalitumainia kanisa la Kipentekoste lituokoe, “sisi tu, miongoni mwa binadamu, maskini kuliko watu wote,” hiyo ni kweli, kwa maana tumepotea. Hiyo ni kweli.

102 Lakini iwapo tunamtumainia Yesu Kristo, basi tumeokolewa, “kwa imani yako,” (nini?) katika kazi iliyomalizika. Na vitu hivi vidogo vinavyotenda kazi, na majina ya kujibandika, havileti tofauti kubwa.

103 Naam, nilimwambia Ndugu Scism, ku-. . .na Ndugu Ness, “Kujibu swali lenu,” nikasema, “naam, siungi mkono upande wo wote wenu ndugu. Nami najua, mradi tu mnazozana, nyote wawili mmekosea. Mnaona? Kwa maana, afadhali nikosee katika fundisho langu, ila niwe sawa moyoni mwangu, kuliko kuwa sawa katika fundisho langu, na nisiwe sawa moyoni mwangu.” Mnaona? Nikasema, “Hata hivyo, ni hali ya moyo wako.”

104 Basi nilijizoeza jambo hilo, kujua jambo hili: ya kwamba, kama mtu, haidhuru anafanya nini, na anatofautianaje, na yale anayosema juu yangu; kama ndani ya moyo wangu, si kwa wajibu tu, bali kutoka moyoni mwangu siwezi kumpenda huyo mtu kama ninavyompenda mtu ye yote yule, basi ninajua kuna kasoro humu ndani, mnaona. Hiyo ni kweli, kwa maana, ni—ni. . .haidhuru kama yeye. . .

105 Maskini ndugu mmoja alikuja, si muda mrefu uliopita, maskini ndugu wa Kanisa la Kristo. Na, loo, alisimama pale, ndipo akasema, “Jamaa huyu ni ibilisi.” Mnaona? Akasema, “Yeye ananena juu ya Roho Mtakatifu.” Akasema, “Hakuna kitu kama hicho. Wale mitume kumi na wawili tu ndio waliompokea Roho Mtakatifu. Na—na kuponya Kiungu kulitolewa tu kwa wale mitume kumi na wawili.” Na akaendelea, kama nusu saa.

106 Ndipo nikasema, “Hebu kidogo, ndugu. Nafikiri inakupasa kunipa tu nafasi kutetea jambo Hili, unaona.” Nikasema, “Ulisema nyinyi mlinena ambapo Biblia imenena, na mlinyamaza mahali iliponyamaza.”

Naye akasema, “Tunafanya hivyo.”

107 Nikasema, “Basi, ulisema wale wanafunzi kumi na wawili ndio tu waliompokea Roho Mtakatifu. Biblia ilisema, ‘Kulikuweko na mia moja na ishirini kwenye chumba cha juu wakati Roho Mtakatifu aliposhuka, wanawake na kadhalika.’ Basi tafadhali niambie, unafikiri Paulo hakuwa na Roho Mtakatifu? Naye alimpokea Huyo muda mrefu baadaye, unaona. Nawe ulisema karama ya kuponya ilitolewa tu kwa wale mitume kumi na wawili. Basi Stefano alishuka akaenda, siku chache baadaye, naye hakuwa mmoja wa wale kumi na wawili. Hata hakuwa mhubiri. Alikuwa shemasi, naye akashuka akaenda Samaria na kuwatoa pepo.” Nikasema. “Loo, ndugu!” Kulikuwa na ukimya hapa, mahali alipopaswa kunyamaza.

108 Ndipo baada ya kumaliza nikasema, “Lakini,” nikasema, “nimekusamehe kwa kuniita ibilisi, maana najua hukumaanisha jambo hilo.”

109 Ndipo alipomaliza, akapanda akaja. Akasema, “Kuna jambo moja ninaloweza kusema. Wewe una Roho wa Kristo.”

110 Nikasema, “Naam, ndugu, mimi ni nani, ibilisi ama wa Kristo?” Unaona? unaona?

111 Bali nawaambia, mnaona, kwa sababu mwanadamu, yeye angeweza kujua kwamba nilimpenda; haidhuru, alikuwa akibishana, na kubishana vikali na kulaumu. Yeye . . .

112 Mimi ni mwindaji, wa wanyama pori, maishani mwangu mwote. Na watu wamesema, “Vipi . . . ” Wakati ule iliponibidi kumuua dubu yule kwa kisu, mnaona. Kasema, “Hivi hukumwogopa?”

113 Nikasema, “La. Kama ningalimwogopa, angaliniua mimi, unaona.”

114 Bali, unaona, huwezi—huwezi kuwapumbaza. Wao wanajua kama unawaogopa, ama huwaogopi. Hebu mwogope farasi, uone vile farasi atafanya, atakukanyaga-kanyaga. Unaona? Kwa hiyo kama unaogopa . . . Huwezi kumdanganya. Huna budi kuwa nao kweli.

Basi hivyo ndivyo ilivyo na Shetani.

115 Hivyo ndivyo ilivyo kati ya watu. Huna budi kuwapenda watu. Huwezi kujisingizia tu. Huna budi kuwa nao, la sivyo sura yako itaonekana mahali fulani, unaona. Hiyo ni kweli. Huna budi kuwapenda watu kweli, nao wanajua unawapenda. Mnaona, kuna kitu fulani juu yake.

116 Ndipo huyo mtu sasa, alimpigia mke wangu simu, siku chache zilizopita, akasema, “Ndugu Branham yuko?”

Kasema, “La.”

117 Kasema, “Vema, jambo moja linalonibidi kusema. Sikubaliani naye, katika theolojia, bali mimi nasema yeye ni mtumishi wa Kristo.”

118 Vema, basi, halafu kabla sijaondoka, alinitumia barua, akasema, “Ninakuja huko, mara utakaporudi. Nataka huo ubatizo wa Roho Mtakatifu unaonena habari zake.”

119 Kwa hiyo, mnaona, mahali tu ambapo ungekuwa . . . Kama ningalikuwa na ile hisi, ya kusema, “Mbona, hufai kitu wewe. Maskini madhehebu yako ya kale hayafai kitu, na—nanyi nyote watu wa Kanisa la Kristo hamfai kitu. Hamfai kitu. Ninyi, ninyi ni mapepo.” Nisingaliweza kumvuta mtu huyo kamwe. Na kama ningalimwambia ya kwamba nampenda, nami sikumaanisha jambo hilo moyoni mwangu, yeye angalitambua vizuri zaidi. Hakuna lingine. Huna budi kulimaanisha moyoni mwako.

120 Vivyo hivyo kwenye siku zile usiku ninapokuja jukwaani chini ya upambanuzi, mnaona. Sifikirii juu ya jambo hilo. Mimi sili chakula kamwe baada ya chakula cha kutwa; ninafunga na kuomba, na kukaa chumbani. Kwa maana, Yeye aliniahidi angefanya jambo hilo. Na kwa hiyo mimi huenda bila uvuli mmoja wa shaka, kwa sababu aliahidi ya kwamba angefanya jambo hilo. Kwa hiyo, mnaona, nini hii yangu. . . najua kusudi langu ni (nini?), nia yangu ni (nini?), kwa ajili ya kuuendeleza Ufalme wa Mungu.

121 Kama mtu akipita njia *hii*, njia *ile*, hata iwe anahudhuria kanisa gani; mradi tu anakuja kwa Kristo, si hoja kwangu. Na hilo liko moyoni mwangu. Mnaona? Na haidhuru, kama tukitoka twende kule na kujiunga na Kanisa la Kristo, hilo ni sawa tu. Hilo ni sawa. Kama yeye. . . Hata ajiunge na kanisa gani, hilo si hoja kwangu. Bali mradi tu niliivuta nafsi yake kwa Kristo, ndilo jambo muhimu.

122 Kwa hiyo, nikasema, "Ndugu Ness, si kusudi niwe tofauti. . ." Sasa nitawaonyesha. . . Ni sawa kutumia *hii*, ndugu? [Huyo ndugu anasema, "Hakika."—Mh.] Nikasema, "Ninataka kusema na kueleza." Na, katika jambo hili, huenda nikawaambia ninyi ndugu hapa. Naam, msilitaje jambo hili miongoni mwa makusanyiko yenu. Kama mkiweza, nifanyieni hisani, he—he—hebu tu niwe ndugu yenu, mnaona. Nami, na iwapo—iwapo nimekosea, basi nisameheni. Bali nataka kuwaelezea, kwa kuwa makundi yote mawili yameketi hapa asubuhi hii, yote mawili Umoja na A—Assemblies, pia, na imani ya utatu.

123 Sasa nataka kutoa tamshi hili. Nataka kusema ya kwamba ninaamini pande zote mbili zimekosea, mradi tu wanabishana mmoja kwa mwingine, kwa maana makusudi yao ni mabaya. Na mradi tu kusudi lako ni mabaya, haidhuru nia yako ni nini, bali kusudi lako kwa nia hiyo ni mbaya, basi jambo hilo halitafaulu kamwe. [Ndugu Branham anapigapiga mimbara mara nne—Mh.] Hiyo ni kweli.

124 Naam, watu wengine wamesema, "Ndugu Branham, wewe ni wa Yesu Pekee." Nataka kusema ya kwamba jambo hilo ni kosa. Mimi si wa Yesu Pekee.

125 Mtu fulani anasema, "Ndugu Branham, wewe ni wa utatu?" La, bwana. Mimi si wa utatu. Mimi ni Mkristo. Unaona? Mimi—ni—mimi si-. . . Neno mtu wa utatu hata halijatajwa katika Biblia, neno "utatu." Wala siamini ya kwamba kuna Miungu watatu mbalimbali.

126 Ninaamini kuna Mungu mmoja katika afisi tatu; Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo sababu hasa tuliagizwa kubatiza katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Ninaamini ya kwamba ni Mungu akijidhili, akishuka.

127 Sasa, Mungu, wakati alipomtokea mwanadamu kwanza, Yeye alikuwa katika mfano wa Nguzo ya Moto. Mnaamini jambo hilo, sivyo? Nini hii . . . Msomaji ye yote wa Biblia anayejua ya kwamba ile Nguzo ya Moto iliyokuwa nyikani ilikuwa Logos, kwamba hiyo ilikuwa yule Malaika wa Agano, ambaye alikuwa ni Kristo.

128 Kwa sababu, Yeye alisema . . . ? . . . Ninaamimi ni Yohana Mtakatifu 6 pale, Yeye alisema, “Ibrahimu asijakuweko,” kasema, “MIMI NIKO.” Yeye alikuwa yule “MIMI NIKO.”

129 Kwa hiyo, huyo alikuwa ni Mungu, mtakatifu; hata kama mtu aliugusa ule mlima, hana budi kuuawa, mnaona. Vema. Naam, Mungu yuyo huyo alikuwa akijaribu kujirudisha katika kiumbe Chake ambacho Yeye aliumba. Naam, Yeye asingekuja karibu nao, kwa maana walikuwa na dhambi, na damu ya mbuzi na kondoo haikuondoa dhambi kamwe. Tunajua jambo hilo. Ilifunika tu dhambi.

130 Naam, lakini basi Mungu yuyo huyo aliyekuwa katika ile Nguzo ya Moto, alifanyika mwili, kupitia kwa Mwanawe, akaishi katika mwili ulioitwa Bwana Yesu Kristo. Biblia ilisema, “Katika Yeye unakaa utimilifu wa uungu kwa jinsi ya mwili.” Naye Yesu alisema katika . . . Vema, katika Timotheo wa Kwanza 3:16, “Bila shaka, siri ya Utauwa ni kuu.” Na kama wao wangeiita kuu, mbona, tungefanyaje sisi, mnaona? “Bila shaka siri ya Mungu ni kuu, Mungu alidhihirishwa katika mwili, na akaonekana na malaika, kisha akachukuliwa juu katika Utukufu,” na kadhalika. Naam, pia Yeye alisema katika Yohana Mtakatifu 14, akamwambia Tomaso, “Ukisha niona Mimi, umemwona Baba. Basi mbona unasema, ‘Utuonyeshe Baba’?” Biblia ilisema, ya kwamba, “Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.”

131 Naam, Mungu hawezi kuwa watu watatu, Miungu watatu, wala Yesu hawezi kuwa Baba Yake Mwenyewe, katika mmoja. Mnaona? Kwa hiyo, mnaona, inafanya yote mawili yakosee kabisa.

132 Sasa kama utaangalia tu, hakuna mahali . . . Kama tuna Miungu watatu, sisi ni makafiri. Naam, tunajua jambo hilo.

133 Kama yule Myahudi alivyoniambia wakati mmoja, nilipokuwa nikizungumza naye, kasema, “Kati ya hao Mungu wenu ni yupi? Ni yupi aliye Mungu wenu: Baba, Mwana, ama Roho Mtakatifu? Wenu ni yupi?”

Nami nikasema, “Mbona, hakuna Miungu watatu.”

134 Akasema, “Hamwezi kumkatakata—kumkatakata Mungu katika sehemu tatu na kisha mumpe Myahudi.”

Nikasema, “La, bwana.” Nikasema . . .

135 Wakati John Ryan alipokuwa ameponywa upofu, pale katika Fort Wayne, mwajua; kisha huyu rabi hapa Mishawa- . . . ama

Fort . . . Benton Harbor. Yeye alisema “Hamwezi kumkatakata Mungu katika vipande vitatu kisha mumpe Myahudi.”

136 Nikasema, “La hasha. Simkati.” Nikasema, “Rabi, lingekuwa ni jambo gumu kwako kuwaamini manabii?”

Akasema, “La.”

137 Nikasema, “Katika Isaya 9:6, yeye alikuwa akinena habari za nani, ‘Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mtoto Mwanamume, ataitwa Mshauri, Mungu Mwenye Nguvu, Mfalme wa Amani?”

Akasema, “Huyo alikuwa ni Masihi.”

Nikasema, “Basi, Rabi, Masihi atakuwa na uhusiano gani na Mungu?”

Akasema, “Atakuwa ni Mungu.”

138 “Hilo ndilo nililofikiria.” Mnaona? Naam, mnaona, hiyo ni kweli kabisa. Hivyo ndivyo alivyo. Na kwa hiyo nikasema, “Niambie sasa ambapo Yesu alishindwa kutimiza yale hasa nabii aliyosema angetimiza.” Ndipo akaanza kulia na kutembea akizunguka. Nikasema, “Kwake Huyo, John Ryan alipata kuona.” Mnaona?

Basi akasema, “Na iwe mbali na Mungu kuwa na mwana.”

139 Nikasema, “Yehova mkuu alimtia uvuli mwanamke, kama nabii alivyosema angefanya, akaumba chembechembe ya damu. Na kwa kupitia chembechembe hiyo ya Damu ndipo ambapo mwili wa Kristo ulikuja.”

140 “Angalia, katika Agano la Kale, Rabi,” nikasema, “mtu alipoenda kutoa dhabihu, alichukua mwana-kondoo. Yeye alijua alikuwa amezivunja amri za Mungu, kwa hiyo akamchukua mwana-kondoo. Akaungama dhambi zake, na huyu mwana-kondoo akauawa. Huku . . . mikono yake ikiwa juu ya mwana-kondoo; kuungama kwake ya kwamba alijua anapaswa kufa kwa ajili ya dhambi zake, bali yule mwana-kondoo alikuwa akipachukua mahali pake. Basi ile chembechembe ya damu ilivunjwa; naye akamshika maskini yule mwana-kondoo kwa mkono wake mpaka aliposikia uhai wake mdogo umemtoka, na amekauka. Ndipo kuhani, bila shaka, akaitupa ile damu mo—motoni, ile madhabahu ya shaba ya hukumu.”

141 Ndipo nikasema, “Mtu huyo, basi, alitoka hapo, akijua ya kwamba mwana-kondoo huyo alikuwa amepachukua mahali pake, ila alitoka akaenda akali na shauku ile ile aliyokuwa nayo alipoingia, unaona, kwa maana haingeondoa dhambi. Mnaona? Lakini, basi, katika kisa hiki, ‘Mwabudu akiisha kusafishwa mara moja, asingejiona tena kuwa na dhambi.’ Huko, kulikuwa na dhabihu iliyotolewa kila mwaka. Lakini,” nikasema, “sasa kuna wakati huu, ‘mwabudu akiisha kusafishwa, asinge kuwa na dhamiri ya dhambi.’ Kwa sababu . . .

142 "Angalia, Rabi. Katika chembe zilizo hai za damu, huo uhai mdogo unaoanza kwenye chembechembe, ambao unatoka kwenye jinsia ya mwanamume, ukaingia kwa mwanamke. Naye mwanamke anatoa yai; lakini, kuku anaweza kutaga yai, bali iwapo hajakuwa pamoja na dume ndege, halitaanguliwa kamwe."

143 Nami nikasema, "Basi Mungu, yule mkuu sana aliyeujaza wakati wote na majira, alishuka akaja kwenye chembechembe hai moja ndogo akaingia kwenye tumbo la uzazi la mwanamke." Kisha nikasema, "Tunapookolewa leo . . . Yesu hakuwa Myahudi wala Mmataifa, kwa maana lile yai liliuzaa tu ule mwili. Ile damu ndiyo iliyokuwa na Uhai. Kwa hiyo sisi—sisi tuna- . . . Biblia ilisema, 'Tunaokolewa kwa Damu ya Mungu.' Mnaona. Yeye hakuwa Myahudi wala mmataifa; Yeye alikuwa Mungu. Kwa hiyo, tunapokuja madhabahuni na kuweka mikono yetu, kwa imani, juu ya kichwa Chake, na kusikia kule kuraruliwa na uchungu mkali pale Kalvari, na kutubu dhambi zetu, ya kwamba tumekosea, Naye alikufa mahali petu!

144 "Basi, unaona," nikasema, "ile damu ya mwana-kondoo isingerudi juu ya huyu, ile damu ambayo . . . Chembechembe yake ilivunjwa, na uhai ulioachiliwa, katika kuvunjwa kwa chembechembe hii ya damu ya mwana-kondoo, usingweza kurudi juu ya mwabudu, kwa kuwa ulikuwa ni uhai wa mnyama, nao usingeungana na uhai wa mwanadamu."

145 "Lakini wakati huu, wakati chembechembe hiyo ya Damu ilipovunjwa, haikuwa ni mwanadamu tu. Huo ulikuwa ni Uhai wa Mungu, uliotolewa. Basi mwabudu anapoiweka mikono yake, kwa imani, juu ya Mwana wa Mungu, na kuungama dhambi zake; si uhai wa mtu mwingine, bali Uhai wa Mungu unarudi ukamwingia mtu huyu, ambao ni Uzima wa Milele. Neno *Zoe*, ambalo linafasiriwa, 'Uzima' wa Mungu Mwenyewe. Naye alisema angetupa sisi Zoe, Uzima wa Milele, na sasa sisi ni wana na binti za Mungu. Haya basi."

146 Nikasema, "Sasa ni kitu gani? Ni Mungu, akijidhili. Yeye alikuja, kwanza; 'hakuna mtu angaliweza kumgusa Yeye,' kwa kuwa mwanadamu alikuwa amefanya dhambi. Kisha alishuka katika mwili, 'kusudi aonje dhambi . . . kuichukua dhambi.' Mnaona, Yeye, jambo pekee ambalo Mungu angalifanya, ili kwamba apate kuwa na haki, ni kufanya jambo hilo namna hiyo."

147 Kwa mfano, vipi kama nilikuwa na mamlaka juu ya kusanyiko hili asubuhi hii, kama yale Mungu aliyokuwa nayo juu ya jamii ya binadamu, nami nikasema, "Mtu wa kwanza anayeitazama nguzo ile, atakufa," ndipo Tommy Hicks akaitazama? Naam, kwa mfano, nimchukue Carl- . . . "Ndugu Carlson, mfie wewe." Hilo halingekuwa jambo la haki. Ningesema, "Leo, wewe ni katibu wangu; mfie." Hilo

lisingekuwa jambo la haki. "Billy Paul, mwanangu, mfie." Hilo si la haki. Jinsi tu ninavyoweza kuwa mwenye haki, ni kupachukua mahali pake mimi mwenyewe.

148 Basi, hivyo ndivyo alivyofanya Mungu. Yeye, Mungu, ni Roho. Naye aliumba . . . Yeye, alibadilisha kinyago Chake. Linapaswa kuwa jambo la kustaajabisha, kwa watu, kufikiri juu ya Yehova mdogo. Yeye angaliweza kuja, akiwa mtu mzima kabisa, bali alikuja kwenye hori, juu ya lundo la samadi. Yehova ndogo, akilia kama mtoto mchanga. Yehova mdogo, akicheza kama mvulana. Yehova mdogo, seremala, kama mfanyi kazi. Yehova mdogo, akiwa kwenye umri wa tineja. Yehova, akining'inia kati ya mbingu na nchi, akiwa na lundo la ute wa walevi na mate ya askari usoni Mwake. Yehova, akiwafia watoto Wake. Yehova, akifa, kusudi akomboe; si mtu mwingine, bali Mungu Mwenyewe! Mnaona, Mungu, hiyo ilikuwa afisi Yake. Kwa nini? Yeye anajaribu kurudi katika moyo wa mwanadamu.

149 Naam, tusingeweza kumgusa Yeye *Pale*. *Hapa*, tulimgusa Yeye kwa mkono wetu. Sasa Yeye alifanya nini, kwa toleo la sadaka ya mwili ule? Yeye amekuwa Yehova *ndani* yetu. Sisi ni sehemu Zake. Kwenye siku ya Pentekoste, ile Nguzo ya Moto ilijipasua Yenyewe, na ndimi za Moto zikakaa juu ya kila mmoja, ikionyesha ya kwamba Mungu alikuwa akijigawanya Mwenyewe miongoni mwa Kanisa Lake.

150 Halafu, ndugu, laiti tungeweza kuungana pamoja, na kuleta jambo Hilo pamoja! Basi tungekuwa na Yehova katika utimilifu, tunapoungana pamoja. Lakini tunawezaje, wakati *huyu* ananena kwa lugha na ana ubatizo, *huyu* naye; halafu kuweka mwali *huu* wa Moto huku, na *huu*? Hebu tuliweke pamoja.

151 Wakati Mungu, kwenye siku ya Pentekoste, aliposhuka, nayo Biblia ilisema, "Ndimi za moto zikakaa juu ya kila mmoja wao." Nao . . . "Ndimi, kama za Moto," miali. Ilikuwa ni ile Nguzo ya Moto ikijitenganisha na ikijigawa Yenyewe, miongoni mwa hao watu, ili kwamba tupate kuwa ndugu. "Siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba, Naye Baba ndani Yangu; Mimi ndani Yangu, nanyi ndani Yangu." Basi, sisi, ni mmoja. Sisi ni mmoja, hatujagawanyika.

152 Naam, Yehova Mungu, *Huku* juu, asingeweza kuigusa jamii ya binadamu, kwa sababu ya sheria Yake Mwenyewe ya utakatifu; Yehova Mungu akawa dhambi kwa ajili yetu, kisha akalipa gharama; ili kwamba Yehova Mungu yeye yule angeweza kuja na kuishi *ndani* yetu. Mungu *juu* yetu; Mungu *pamoja* nasi; Mungu *ndani* yetu. Si Miungu watatu; Mungu mmoja! Maprofesa wanapata kichaa, wakijaribu kuliwazia jambo hilo. Ni—ni ufunuo. Halina budi kufunuliwa kwako.

153 Naam, sasa, inapofikia ubatizo, sasa, watu wengi . . . Naam, hamna budi kufanya jambo hilo, enyi ndugu. La sivyo, ni

kama nilivyomwambia Ndugu Scism na kwa Ndugu Ness, ya kwamba kama ninyi...U—ubishi ulizuka. Na ye yote, wengi wenu wanachuoni hapa mnafaa kuliko mimi; bali nimesoma sana hilo somo. Na nimesoma wale Mapadri Waliotangulia Nikea, Baraza la Nikea, na wanahistoria wote, na kadhalika.

154 Hoja hiyo ilitokea kwenye lile Baraza la Nikea. Pande zote mbili ziliharibika; wakati kanisa Katoliki lilipochukua msimamo uliopita kadiri wa utatu, nao ule mwingine ukaingia katika umoja, na pande zote mbili zikaenda kombo. Kweli kabisa, kwa sababu mwanadamu alifanya jambo hilo.

155 Inakupasa kumwacha Mungu atende jambo hilo, wala hakuna haja kwetu sisi kujaribu kuliwazia. Hebu tuwe ndugu. Hebu tuendelee tu na tumwache Mungu afanye jambo atakalofanya. Kama Yeye ni asiye na kikomo na anajua mambo yote, naye alibashiri mwisho tangu mwanzo, tunawezaje kufanya jambo lo lote juu yake? Endelea tu kusonga mbele. Hiyo ndiyo njia. Piga hatua, kama nilivyosema jana usiku, pamoja na Yoshua wetu aliye mkuu.

156 Sasa angalia, kama kuna Miungu watatu...Nataka tu kuwaonyesha jinsi hili lilivyo la kipuzi. Kama kuna Miungu watatu, basi Yesu alikuwa Baba Yake Mwenyewe...Yesu asingekuwa Baba Yake Mwenyewe, akiwa mmoja. Na, iwapo wako watatu, Yeye hakuzaliwa kibikira. Sasa ni wangapi... [Ndugu Branham anaeleza, akitumia vitu vitatu—Mh.] Nitasema *hiki* ni Mungu Baba; na *hiki*, ni Mungu Mwana; na *hiki* ni Mungu Roho Mtakatifu.

157 Sasa, kwenu ninyi ndugu mbalimbali hapa, hebu angalieni jambo hili kwa dakika moja muone kile ninachojaribu kuonyesha. Naomba ya kwamba Mungu atawajalia mlione. Basi, angalieni, nyote wawili mnaamini jambo lile lile, bali Ibilisi ameingia tu kati yenu na kuwatenganisha juu ya jambo hilo. Ni jambo lile lile hasa, nami nitawathibitishia ninyi, kwa msaada wa Mungu, na kwa Biblia ya Mungu. Iwapo si Biblia, basi msilipokee. Hiyo ni kweli.

158 Lakini sasa angalieni. [Ndugu Branham anaeleza, akitumia vitu vitatu—Mh.] *Hiki* ni (nini?) Mungu Baba; *hiki* ni Mungu Mwana; *hiki* ni Mungu Roho Mtakatifu. Vema, sasa, hebu tukome sasa kwa muda kidogo tu, tukiviweka hivyo vitatu kule; Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

159 Loo, si—sitapata wakati wa kufanya jambo hili. Ni-... [Ndugu wanasema, "Endelea! Endelea!"—Mh.] Lakini, mnaona, vema, nitaharakisha tu upesi niwezavyo. Samahani, ndugu zanguni, bali si—si—sijapata kuzungumza nanyi, nami na—nataka kufanya jambo hili.

160 Halafu basi, angalieni; Mungu Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Naam, ni Nani aliyekuwa Baba wa Yesu Kristo?

Mungu ndiye aliyekuwa Baba wa Yesu Kristo. Sote tunaamini hilo. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema.

161 Sasa, tunapochukua Mathayo 28:19, wakati Yesu aliposema, “Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” Siku kumi baadaye, Petro alisema, “Tubuni, mkabatizwe katika Jina Lake Bwana Yesu Kristo.” Kuna hitilafu dhahiri mahali fulani. Naam, hebu tusi-. . . kuna . . .

162 Kila mtu amekwisha toa ushuhuda, na kadhalika. Hii hapa. Hivi ndivyo ninavyoamini, nami ninaliweka tu mbele zenu, ndugu. Sisemi jambo hili huko nje mimbarani; ni juu yenu. Bali nataka kuwaonyesha jambo ninaloona pande zote mbili, ili kwamba Roho Mtakatifu awafunulie jambo hili, mnaona.

163 Naam, Mathayo 28:19, na iwapo—iwapo Mathayo 28:19 inahitilafiana na Matendo 2:38, basi kuna hitilafu katika Biblia, nayo haina thamani hata ya karatasi iliyoandikiwa.

164 Sasa kama mtaangalia katika Mathayo sura ya 16, Yesu alimpa Petro ufunuo, kisha akampa Yeye zile funguo.

165 Sasa, kumbuka, Biblia haifunuliwi kwa theolojia ya taratibu za kujibunia. Haifunuliwi. Ni ufunuo.

166 Ilikuwa ni ufunuo, kwanza. Kwa nini Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko ya Kaini? “Ilifunuliwa kwake,” ya kwamba haikuwa embe, na matofaa, na machungwa, na matofaa. Kama matofaa yatawafanya wanawake watambue wao wako uchi, afadhali tuwape matofaa tena, ndugu. Si mnafikiri hivyo? Sasa, hilo, hilo linasikika la kukufuru, bali simaanishi kusema hivyo. Lakini, haikuwa matofaa. La, bwana. Basi, na kama hivyo ndivyo ilivyo, basi, “Habili alifunuliwa,” ya kwamba yeye alikuwa damu ya babaye. Kwa hiyo alitoa damu, kwa sababu ilikuwa ni ufunuo. Jambo zima limejengwa juu ya huo.

167 Sasa angalia, huyu hapa mzee mvua samaki asiye na elimu, hata hana elimu ya kutosha . . . Biblia ilisema alikuwa asiye na elimu wala maarifa. Bali alikuwa amesimama pale, ndipo Yesu akauliza lile swali, “Mnasema Mimi Mwana wa Adamu kwamba ni nani?”

168 “Mmoja akasema, mbona, Wewe ni—Wewe ni ‘Musa.’” Wao wanasema wewe ni ‘Musa.’” Wao, nini hii . . . wanasema, na mmoja akasema, mbona, wewe ni ‘Yeremia, ama manabii,’ na *hivi*, *vile*, na *vinginevyo*.”

169 Yeye akasema, “Hilo silo swali. Niliwaulizeni *ninyi*. Ninyi mnasema kwamba Mimi ni nani?”

170 Ndipo Petro akajitokeza moja kwa moja, akasema, “Wewe ni Mwana wa Mungu.”

171 Ndipo akasema, “Heri wewe, Simoni, Bar-yona.” Sasa angalia. “Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni.” Mnaona?

172 Sasa tazama, sasa, kanisa Katoliki linasema ya kwamba Yeye alilijenga kanisa juu ya Petro. Hilo ni kosa.

173 Kanisa la Kiprotestanti linasema Yeye alilijenga juu Yake Mwenyewe. Bali sasa angalia uone, uone kama ndivyo ilivyo.

174 Yeye alilijenga juu ya ufunuo wa kiroho wa Yeye alikuwa ni Nani, mnaona, kwa sababu Yeye alisema, "Heri wewe Simoni, Bar-yona. Mwili na damu havikukufunulia hili. Nasema wewe ndiwe Simoni; juu ya mwamba huu" (mwamba upi? huo ufunuo) "nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda." [Ndugu Branham anagonga mimbara mara tatu—Mh.]

175 Ndipo, wakati Petro alipokuwepo wakati Mathayo 28 iliponukuliwa, kisha akageuka, siku kumi baadaye, akiwa na ufunuo huo, na kubatiza katika "Jina la Bwana Yesu Kristo." Kwa nini alifanya jambo hilo? Kwa ufunuo wa Mungu; naye alikuwa na zile funguo za Ufalme, ndugu.

176 Sasa huenda nikawaudhi kwa muda kidogo, upande wenu mmoja, lakini tulieni kwa muda kidogo. Hakuna mahali pamoja katika Biblia ambapo mtu ye yote aliwahi kubatizwa katika Jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Hakuna mahali pamoja katika Maandiko. Na iwapo pako, patoeni. Na kama mnaweza kupata mahali po pote katika historia takatifu, mpaka kule kuundwa kwa kanisa Katoliki, nawatakeni mpatoe. Hakuna mahali, sasa, na hiyo ni kweli.

Lakini sasa ngojeni kidogo, enyi wa Umoja, hebu kidogo.

177 Naam, hakuna mahali ambapo... Kama mtu ye yote anaweza kunionyesha fungu moja la Maandiko ambapo ibada hiyo ilitumiwa katika Biblia, ya "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," unawajibika kuja kuniambia ambapo mtu fulani alibatizwa namna hiyo.

178 Na baadhi yao wanasema, "Vema, nitachukua aliyosema Yesu, si aliyosema Petro." Kama wao walihitilafiana, mmoja kwa mwingine, tutafanya nini? Kama yote si Mungu, ni sehemu gani ya Biblia iliyo sahihi?

179 Yote haina budi kulingana na kushikana, na ni ufunuo tu wa Mungu. Mashule yetu hayatafundisha jambo hilo kamwe. Ni ufunuo, ambao huna budi kuuona.

180 Halafu, iwapo watu hao wawili walihitilafiana, mmoja kwa mwingine, basi tunasoma Biblia ya namna gani? Ninajuaje kama Yohana 14 ni kweli, ama si kweli? Ninajuaje kama Yohana 3 ni kweli, ama si kweli? Je! je! nitajua? Mnaona?

181 Bali njia pekee ambayo ninaweza kuwa na imani katika Mungu, ni kujua ya kwamba Biblia ile ni kweli, na kuamini ni kweli, na kudumu Nayo. Ingawa siifahamu, ninaifuata, haidhuru.

182 Lakini wakati hitilafu hizi zinapozuka, ndipo ninaenda mbele za Mungu, na kutafuta nijue. Ndipo Malaika yule yule anayekutana nami katika mikutano, na usiku, Ndiye Ambaye alinifundisha Hili. Mnaona? Sasa angalieni kama jambo hili ni kweli, jinsi hili lilivyo sasa.

183 Basi, Mathayo 28:19, hebu tuangalie kwa muda kidogo sasa. Basi sasa nitachukua Matendo 2:38 papa hapa, ambapo Petro alisema, "Bwana Yesu Kristo." Naye Mathayo akasema, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu."

184 Sasa sikilizeni. Yeye alisema, "Mkawabatize . . . " Si "katika Jina la Baba, katika Jina la Mwana, katika Jina la Roho Mtakatifu." Kamwe hakusema hivyo. Hakuna "jina . . . katika jina . . . katika jina."

185 Hakusema kamwe, "Mkawabatize katika *majina* ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," kwa sababu hata si la busara.

186 Alisema, "Mkawabatize katika Jina (J—i—n—a) la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] " . . . la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," kiunganisho "na, na, na."

187 Si "majina." Si "katika Jina la Baba, Jina la Mwana, Jina la Roho Mtakatifu." Si, "katika *majina* ya Baba, Mwana, na Roho mtakatifu. Bali "katika Jina," J-i-n-a, umoja, "la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Basi ni lipi kati yake lililo jina la kweli la kubatiza? Ni Jina moja. Ni lipi? Je! "Baba" ndilo jina la kweli, ama Mwana ndilo jina la kweli, ama Roho Mtakatifu ndilo jina la kweli?

188 Ni "Jina," mahali fulani. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko,—"Amina."—Mh.] Vema, sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani, basi. Kama lile "Jina," basi, kama Yesu alisema, "mkawabatize katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu . . . " Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yesu alisema hivyo? ["Amina."] hayo ni Maandiko. Ni Mathoyo 28:19, "Katika Jina la Baba, Mwana . . . "

189 [Ndugu Branham anaona kukatizwa—Mh.] Ni jambo ambalo sisi . . . La, ni, nilifikiri . . . Sawa, bwana. [Ndugu fulani anasema, "Tafadhari, Ndugu Branham?"] Naam. [Nataka kugeuza kanda hii upande wa pili, nami sitaki kutoyanasa."] Vema. [Mhali patupu kwenye kanda.]

190 Basi, "katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Sasa sikilizeni ndugu. Hakuna kitu kama jina la "Baba," kwa maana Baba si jina. Ni cheo. Hakuna kitu kama jina la "Mwana," maana Mwana ni cheo. Hakuna kitu kama jina la "Roho Mtakatifu." Hivyo ndivyo alivyo Yeye.

191 Nilikuwa nikisema jambo hilo kwenye kifunguakinywa cha wahudumu asubuhi moja, ndipo mwanamke mmoja . . . akikiuka utaratibu bila shaka, mtu ye yote ambaye angekatiza, kitu kama

hicho. Akasema, "Ngoja kidogo! Samahani!" Kasema, "Roho Mtakatifu ni jina."

192 Nikasema, "Hivyo ndivyo alivyo Yeye. Mimi ni mwanadamu, bali jina langu si 'Mwanadamu.'"

193 Ni Roho Mtakatifu! Hilo si jina. Hivyo ndivyo alivyo Yeye. Ni jina la kitu, bila shaka, bali si nini hii . . . Ni—ni nini hii . . . si jina.

194 Sasa, kama Yeye alisema, "Mkawabatize katika Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu"; na wala Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu si jina, basi hilo Jina ni lipi? Tunataka kutafuta kujua.

195 Naam, tunaweza kulipata lote katika mahali pamoja hapa, kama tu mkiangalia na—na—na kutumia wakati mdogo sasa, ama kuokoa wakati mdogo, ndivyo nilitaka kusema. Sasa angalia Mathayo 28:19. Sasa, sisemi kwamba . . .

196 Huenda ninyi, huenda ikawa mlifanya jambo hilo, baadhi yenu dada ama ndugu. Pengine mlichukua kitabu fulani, siku moja, mkaangalia mwisho wake, na kusema, "Yohana na Maria wakaishi kwa furaha baadaye." Vema, Yohana na Mariamu ni nani? Ni nini, Yohana na Mariamu ni nani walioishi kwa furaha baadaye? Kuna njia moja tu utakayojua Yohana na Mariamu ni akina nani; hiyo ni, kama ni fumbo kwako, rudi nyuma ukakisome hicho kitabu. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Rudi nyuma mwanzoni ukakisome chote, nacho kinakwambia Yohana na Mariamu ni nani.

197 Vema, kama Yesu alisema, Yesu Kristo Mwana wa Mungu, ambaye alisema, "Basi enendeni, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," na wala *Baba*, *Mwana*, ama *Roho Mtakatifu* si jina. Basi, iwapo ni fumbo, inatupasa kurudi katika mwanzo wa hiki Kitabu.

198 Basi hebu tugeuke kwenye sura ya kwanza ya Mathayo, nasi tutaanza pale, inatoa ukoo, hata inapofikia aya ya 18.

199 Sasa angalia, sasa angalia kwa muda kidogo tu. [Ndugu Branham anaeleza, akitumia vitu vitatu—Mh.] *Hiki* ni Baba, mkono wangu wa kushoto; *hiki* katikati ni Mwana; na *hiki* ni Roho Mtakatifu. Naam, *hiki* ni Baba wa Yesu Kristo. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Mungu ndiye Baba wa Yesu Kristo. Sote tunaamini jambo hilo? ["Amina."] Vema.

200 Sasa Mathayo 1:18 ilisema:

> *Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi. Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla* yeye . . . *hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa . . .*

201 [Ndugu Branham ananyamaza kidogo. Kusanyiko linasema, "Roho Mtakatifu."] Nilifikiri *Mungu* ndiye Baba Yake. [Ndugu Branham ananyamaza kidogo—Mh.]

Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake YESU, . . .

Naye Yusufu, mumewe, kwa vile alikvyokuwa mtu wa haki, . . . hakutaka *kumwaibisha*, bali *aliazimu kumwacha kwa siri.*

Hivi, *basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo: maana mimba yake ni kwa uweza wa* . . .

202 [Ndugu Branham ananyamaza. Kusanyiko linasema, "Roho Mtakatifu."] Nilifikiri Mungu ndiye aliyekuwa Baba Yake. Basi, hivi yeye ana baba wawili, ndugu? ["La."—Mh.] Hawezi kuwa nao. Kama alikuwa nao, Yeye alikuwa mwana haramu, nasi tuna dini ya namna gani pale? Hamna budi kukubali ya kwamba Mungu Baba na Roho Mtakatifu ni Roho yule yule. Bila shaka, ndivyo ilivyo. Hakika, ni Roho yule yule. Naam, tuendelee mbele, tupate kuona jambo hilo.

Naye atamzaa mwana, nawe utamwita jina lake YESU, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi yake.

. . . Hayo yote *yamekuwa, ili litimie* . . .

203 Ninayanukuu Maandiko. Ninyi wahudumu mnajua, ninapoendelea

. . . *ili litimie* . . . *lilonenwa na Bwana kwa* nabii akisema,

. . . *bikira atachukua mimba, naye atamzaa mwana; nao watamwita jina lake Imanueli*; ambalo tafsiri yake ni, . . .

204 [Ndugu Branham ananyamaza kidogo. Kusanyiko, "Mungu pamoja nasi."] "Mungu pamoja nasi!" Hiyo ni kweli? ["Amen."—Mh.]

205 Basi Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni lipi? [Ndugu fulani anasema, "Yesu Kristo."—Mh.] Vema, bila shaka. Hiyo ndiyo sababu Petro aliwabatiza katika Jina la "Yesu Kristo."

206 Lakini, sijali, kama umebatiza katika jina ya Ua la Uwandani, Ninyoro ya Mabondeni, ama Nyota ya Asubuhi, hizo ni vyeo, pia. Kama moyo wako ni sawa mbele za Mungu, Yeye anaujua moyo wako.

207 Lakini sasa, basi, nilitamka jambo hilo. Sasa, sasa nilisema . . . Sasa Ndugu Scism alisema, "Naam!" Bila shaka, hakika, hilo lilionekana kama Umoja, kwa hiyo alirukia jambo hilo mara moja.

208 Basi nikasema, "Sasa hapa nataka kuwaambieni jambo fulani sasa." Mnaona? Nikasema, "Basi nataka kuwathibitishia ya kwamba, watu hawa wawili, walisema jambo lile lile."

209 Sasa, Mathayo alisema, "Katika Jina la Baba." Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sawa. Naye Petro akasema, "Katika Jina la Bwana." Mathayo 28:19 ilisema, "Katika Jina la Baba," na Matendo 2:38 ilisema, "Katika Jina la Bwana.'" Daudi alisema, "Bwana alimwambia Bwana wangu" Ilikuwa ni Nani? Baba na Bwana ni jina lile lile. Daudi alisema, "Bwana alimwambia Bwana Wangu, 'Keti upande wa mkono Wangu wa kuume.'" Mnaona? "Katika Jina la Baba; katika Jina la Bwana."

210 Halafu Mathayo akasema, "Katika Jina la Mwana," naye Petro akasema, "Katika Jina la Yesu." Mwana ni nani? Yesu.

211 "Katika Jina la Roho Mtakatifu," ilikuwa ni Mathayo; ndipo Petro akasema, "Katika Jina la Kristo," yule Logos.

212 *Baba, Mwana, Roho Mtakatifu*, "Bwana Yesu Kristo." Mbona, ni kamilifu iwezavyo kuwa. Mnaona?

213 Ndugu Scism akaniambia. Ndugu Scism, yule ndugu wa Umoja, akasema, "Ndugu Branham, hiyo ni kweli, ila" akasema, "lile ndilo *hili*."

214 Nikasema, "Basi hili ndilo *lile*." Hiyo ni kweli. Mnaona? Nikasema, "Iwapo lile ndilo *hili*, hili ndilo *lile*. Kwa hiyo mnazozania kitu gani?"

215 Nikasema, "Hebu niwape shauri, ndugu. Kama nikiwahi kumbatiza mtu, ningembatiza hivi . . . "

216 Nikasema, "Huyu hapa Dk. Ness." Na mtu fulani alisema muda mfupi uliopita, ninyi ndugu, ya kwamba mlijua Dk. Ness.

217 Vema, nitasema, hapa, Ndugu Hicks, hapa, yeye ana-. . . nafikiri una Digrii ya Daktari. Sivyo? Vema.

218 "Basi nikasema, "Kama Dk. Ness, anayeketi hapa . . . " Sasa nikasema, "Kama nilitaka . . . " Naam, ninapompeleka mtu majini kuwabatiza, ninazitambua kama tu alivyofanya, nikasema, "Hizo vilikuwa ni vyeo vilivoambatana na Jina Lake."

219 Nikasema, "Sasa, ndugu wa Assemblies wanatumia vyeo, na wa Umoja wanatumia Jina." Nikasema, "Basi nitawathibitishia, nyote wawili wamekosea, nami niko sahihi." Unajua jinsi itakubidi . . . Ukiwa na watu waliochoka akili namna hiyo, huna budi kuwa mchekeshaji mara kwa mara, kusudi kwa namna fulani uwachangamshe kidogo. Kwa hiyo nikasema, "Nitawathibitishia ya kwamba nyote wawili mmekosea, nami niko sahihi."

220 Nikasema, "Sasa vipi kama nilitaka kumheshimu Ndugu Ness, ningesema . . . "

221 Ama, ama Ndugu Hicks hapa, mnaona. Ningesema, "Hicks!" Naam, hilo lingesikika sawa? La. Vema, vipi kama ningesema, "Daktari! Wewe Dakt! Na hivyo je?" Sasa, hilo linasikika kama dharau, sivyo?

222 "Vema," nikasema, "hivyo ndivyo ninyi wa Assemblies mnavyofanya, mnaona. Wakati ninyi ndugu wa Assembly mnaposema, 'Katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu,' mnasema tu, 'Katika jina la kasisi, daktari.'"

223 Kisha nikasema, "Halafu, ninyi ndugu wa Umoja, mnapobatiza, mnasema, 'Yesu!'" Wao hawatumii . . .

224 Wao . . . Yesu Pekee, wanatumia tu jina "Yesu." Kuna Yesu wengi. Bali, ni Bwana Yesu Kristo, mnaona. Kuna wengi . . . Wanaobatiza katika jina la "Yesu," bila shaka sikubaliani na jambo hilo; hakuna Andiko. Chukueni ya asili, muone kama si "Bwana Yesu Kristo." Bila shaka, Yeye ni Bwana Yesu Kristo. Kuna Yesu wengi, bila shaka. Naye *Kristo* ni "Aliyetiwa Mafuta."

225 Nami nikasema, "Naam, kama nilikuwa nikitaka kumwambia Ndugu Ness jambo lile lile. Ningesema, hivi lingesikika sawa kwangu kusema, 'Wee, Ness!'?" Nikasema, "Hivyo ndivyo ninyi wa Umoja mngesema jambo hilo. Mnaona? Si huko ni kumdharau mtu huyo ambaye amesoma, naye ana Digrii ya Juu Sana? Iwapo amesoma kwa bidii kuipata, anapaswa kupewa cheo chake."

226 Kisha nikasema, "Ndipo kama ningesema, 'Wee, Dakta!'" Nikasema, "Hivi hilo halingalisikika lisilopendeza, kwa mhudumu kumwita mwingine namna hiyo?" Ama, nikasema, "Hivyo ndivyo tu mnavyolifanya jambo hilo, upande tu wa hivyo vyeo."

227 Lakini nikasema, "Ninapompeleka mtu majini; ninatembea kule na kumwuliza, na kuzungumza naye, ninapata jina lake kwamba yeye yu nani, na imani yake.

228 "Ndipo ninaomba, na kusema, 'Sasa, Baba, kama vile Wewe ulivyotuagiza kwenda ulimwenguni kote na kuwafanya mataifa yote wanafunzi . . ."'" Ninyi ndugu mnajua ya kwamba hilo ndilo la asili, mnaona. "'" . . . kuwafanya mataifa yote wanafunzi, mkiwabatiza katika Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu; mkiwafundisha kuyashika mambo yo yote" ambayo Wewe ume- . . . mambo yote ambayo Wewe umetufundisha.'

229 "Kwa hiyo basi nikasema, 'Kwa kuungama imani yako; kwa kuungama dhambi zako, na imani yako katika Mwana wa Mungu, nakubatiza, ndugu yangu mpendwa, katika Jina la Bwana Yesu Kristo.'"

230 Nikasema, "Hivyo ndivyo ninavyobatiza. Ninatambua vyeo Vyake, alichokuwa, zote Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Na sababu ya Yesu kusema jambo hilo, ilikuwa . . . "

231 Sasa angalieni. Kama jambo hilo si kweli, mna hitilafu katika Maandiko; mna hitilafu. Nanyi mtafanya nini wakati . . . Vipi kama ndugu huyu Mbudha angesimama na kusema kwamba, "Na *hili* je?" Wangesemaje na huku waliniambia . . .

232 Kule, wakati ndugu huyu wa Kihindi alipomsai Morris Reedhead, akamwambia, kasema, “Na Marko 16 je?” Ilimbidi kujikokota juu ya jambo hilo.

233 Haikubidi kujikokota juu ya jambo lo lote. Hilo ni Neno la Mungu. Dumu Nalo. Omba tu. Pata ufunuo. Lote ni sawa.

234 Mnaona, wote wawili wanasema jambo lile lile, sasa; si vyeo; la kabisa. Nikasema, “Basi . . . ”

235 Ninamtambua Yeye. Yeye alikuwa Baba; si Mungu mwingine. Alikuwa Mwana; si Mungu mwingine. Mungu yeye yule! Ni afisi tatu. Mungu katika majira ya Ubaba, kama mkitaka kuyaita, ya Ubaba; Uwana; na ni Mungu yeye yule ndani yetu sasa. “Nitakuwa pamoja nanyi.” Kile “Nitakuwa,” kijina cha nafsi, “Nitakuwa pamoja nanyi.” Kwa hiyo, mnaona, ni afisi tatu, si Miungu watatu.

Naam, ndugu, kama hao wanafunzi hawakuzitumia, na kote kote . . .

236 Mimi sisemi lo lote dhidi yake. Hilo ni sawa. Bali nawaambia, kama mtu alikuja huku nje, naye alikuwa amebatizwa katika jina la “Ua la Uwandani, Ninyoro ya Mabondeni, na Nyota ya Asubuhi,” naye alimwamini Yesu Kristo kama Mwokozi wake; ningesema, “Mungu akubariki, ndugu! Njoo, hebu twende!” Mnaona? Hiyo ni kweli. Sababu, kama moyo wako si sawa, wewe si sawa, hata hivyo. Kweli kabisa. Na mo—moyo wako hauna budi kuwa sahihi.

237 Ndipo nikasema, “Basi, angalia. Sasa, kama nilikuwa naenda kumsalimia Ndugu Ness hapa, ningesema ‘Kasisi Daktari Ness.’ Hiyo ni sawa kabisa. Yeye ni mhudumu. Anapaswa kuchukuliwa kama kasisi. Yeye amesoma, akapata elimu nyingi. Ana Digrii ya Daktari, kwa hiyo hana budi kuitwa ‘daktari.’ Hicho ni cheo chake, mnaona. Na jina lake ni ‘Ness,’ hata hivyo. Naam, nisingesema, ‘Wee, Ness! Wee, Dakta!’ La, hilo lisingekuwa sawa. Ningesema, ‘Kasisi Daktari Ness.’

238 “Mnaona, hivyo ndivyo ninavyomwita, mnaona, alivyo Yeye; vyote Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ‘Bwana Yesu Kristo.’” Mnaona?

239 Basi nikasema, “Kama nikipata kumbatiza mmoja huko nje katika makanisa yenu yote, hivyo ndivyo nitawabatiza.” Nikasema, “Je, ungempokea huyo, Ndugu Ness?”

240 Akasema, “Bila shaka. Yeye amebatizwa katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.”

Nikasema, “Ungempokea huyo, Ndugu Scism?”

Akasema, “Bila shaka, yeye amebatizwa katika Jina la Yesu.”

241 Nikasema, “Basi imekuwaje kwenu, enyi ndugu? Mbona msikubali jambo hilo, kisha mvunje kuta hizi waliko maskini

wanadamu hawa. Wa Umoja wanataka, kweli, makusanyiko, wanataka kuabudu pamoja na Waassemblies. Nalo la Assemblies, kusanyiko lenyewe, linataka kuabudu pamoja la wa Umoja. Nao hawa ndugu wako namna hiyo. Wako namna hiyo. Bali mradi tu ibilisi anaweza kuwafanya wapigane . . . ”

242 Sasa mnaona ninalomaanisha, ndugu? Ninaelekeza kwenye jambo hilo moja, Yesu Kristo, na kuungana kwa Mwili wa Yesu Kristo. Hilo ndilo kusudi langu. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

243 Naam, sisemi kitu juu ya "Kube, wewe hujabatizwa katika Jina la Yesu; unaelekea kuzimuni!" Naam, huo ni upuzi.

244 Nitawaambia kilichotukia juzijuzi. Nilikuwa huko chini Texas. Kabla ya kuondoka . . . Nao ndu—ndugu hapa ni mashahidi wa jambo hili. Kanisa la Umoja, makanisa sabini na mawili, waliudhamini mkutano wangu. Nami nikamweka Ndugu Petty, yule ndugu wa Assemblies, jukwaani usiku huo. Naam, mnajua jambo hilo ni kweli. Yeye ni ndugu wa thamani, Ndugu Petty, kama ye yote wenu anamjua, kutoka Beaumont, Texas. Ni mmoja wa watu wazuri sana niliopata kukutana nao. Mkewe ni Mkatoliki aliyeongoka, mwanamke mtauwa hasa. Yeye ni mtu halisi wa Mungu.

245 Niambieni ni nani aliye mtu bora kuliko Roy Wead, wa Assemblies of God. Tajeni ye yote wa watu hawa, angalieni hapa, ndugu hawa wote ninaowajua kutoka hapa. Ndugu kutoka kanisa la Filadelfia hapa, na watu wa Assemblies of God, basi ni watu gani walio bora zaidi? Niambieni ni wapi. Niambieni ni mtu gani aliye bora kuliko Jack Moore? Niambieni hilo. Yeye ni wanachokiita . . . Wao ni wafuasi wao. Yeye si mshupavu wa dini. Unawapata washupavu wa dini pande zote mbili; na huko ndiko watu wanakoelekeza kidole, na huko ndiko Ibilisi anakoelekeza.

246 Bali hao wote ni watu wa Mungu. Mungu amewapa Roho Mtakatifu. Isingalikuwa ni kwa neema ya Mungu, sote tungekuwa tumepotea, na mizozo yetu na kadhalika. Hiyo ni kweli kabisa. Bali neema ya Mungu inatuunganisha pamoja. Si ajabu tunaweza kuimba, "Kibarikiwe kifungo kiifungacho mioyo yetu katika upendo wa Kristo." Hilo ndilo tunalohitaji, basi.

247 Na kwa hiyo mnajua nini? Kiongozi Mkuu wa ka—kanisa, aliniita, akasema, "Ulijua ulilofanya jana usiku?" Usiku wangu wa pili kule.

Nikasema, "Ati nini?" Nikasema, "Tulikuwa na mkutano wa ajabu."

Kasema, "Ulikuwa na mtu kwenye mimbara yako aliyekuwa mwenye dhambi."

Nikasema, "Sikujua hilo." Alikuwa . . .

Kasema, "Yule Bw. Petty."

248 "Lo!" nikasema, "ati mwenye dhambi? Mbona," nikasema, "yeye ni mhubiri wa Assemblies of God, ndugu."

249 Akasema, "Naam, lakini yeye angali ni mwenye dhambi, kwa maana hajabatizwa sawasawa."

250 Nami nikasema, "Ndugu, naomba uniambie kwa nini." Nikasema, "Yeye ana Roho Mtakatifu."

251 Akasema, "Ndugu Branham, Petro alisema nini? 'Tubuni, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu.' Kwa hiyo dhambi zako haziwezi kuondolewa mpaka umebatizwa katika Jina la Yesu."

Nikasema, "Hiyo ndiyo kanuni, ndugu yangu?"

Akasema, "Hiyo ndiyo kanuni."

252 Nikasema, "Mungu basi alipindua gari Lake Mwenyewe la matofaa basi, katika Matendo 10:49, kwa kuwa, 'Petro alipokuwa akisema maneno hayo, Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile Neno,' mnaona, nao hawakuwa wamebatizwa, kamwe. Basi, Mungu aliwapa Roho Mtakatifu watu ambao hata hawakuwa wameongoka?" Nikasema, "Unasimama wapi sasa basi?"

253 Akasema, "Unajua tutakalofanya?" Kasema, "Tunachora duara dogo, na kukuacha moja kwa moja nje ya mviringo wetu."

254 "Basi," nikasema, "mimi nitachora mwingine, na kuwavuta ndani moja kwa moja tena." Nikasema, "Huwezi kuniacha nje, maana ninawapenda. Mnaona, hamwezi kufanya hivyo kamwe." Nikasema, "Kuna wengi sana wa ndugu ze—zenu huko nje wanaonipenda mimi na wananiamini." Nikasema, "Ninyi, nita—nita-. . . Wao watakuja, hata hivyo." Nikasema, "Watakuja. Wala hamwezi kuniacha nje. Kama mkiniacha nje, mimi nitawavuta ndani tena." Nikasema, "Mnapochora mviringo mmoja, Mungu, kwa neema Yake, atanijalia kuchora mwingine na kuwaingiza moja kwa moja ndani tena." Hiyo ni kweli, kuwarudisheni moja kwa moja ndani tena.

255 Basi, ndugu, loo, katika Jina la Kristo hebu niseme jambo hili. Ni—nina-. . . Najua nawachelewesha hapa; na karibu imekaribia sana wakati wa kufunga, nadhani, lakini hebu niseme tu jambo hili, mnaona.

256 Ndipo nikamwambia mtu huyo, nikasema, "Ningeabatana nawe mradi tu ungehubiri Maandiko, na uwe na upendo, na uamini ya kwamba hayo. . .na uhubiri na useme ulikuwa unawabatiza watu. . .si katika Jina la "Yesu," Yesu pekee. La, bwana. Hakika ni—nisingekubaliana na jambo hilo, kwa maana mimi ninawajua Yesu kadha; ninawajua katika Afrika na mahali mbalimbali, watu wanaoitwa Yesu. Bali kama ukitumia msemo wa 'Bwana wetu Yesu Kristo,' nitakubaliana nawe juu ya jambo hilo. Hiyo ni sawa. Nitaandamana nawe. Nafikiri inakubidi

kuweka 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu' kwanza, unaona" kulipata vizuri." Nikasema, "Nafikiri unapaswa kufanya hivyo."

Lakini akasema, "Loo la, la! Hivyo ni kurudi kwenye utatu."

Nikasema, "Si utatu, ni Mungu mmoja katika afisi tatu!"

257 Si utatu, wa Miungu watatu. Hatuna Miungu watatu. Bila shaka hatuna. Hakuna kitu kama hicho. Haukufundishwa katika Biblia. Na kuna Mungu mmoja tu. "Sikilizeni, enyi Israeli, Mimi ni Bwana Mungu wenu." Mungu mmoja! Amri ya kwanza, "Usiwe na miungu wengine mbele Zangu." Bila shaka, Yeye ni Mungu mmoja, si watatu.

258 Hiyo ni tafsiri ya Kikatoliki ya jambo hilo; na lilitolewa kwa Katoliki likaingizwa kwa Waluteri, na kuendelea, na kadhalika, na inaaminiwa sana-sana miongoni mwa watu leo ya kwamba tuna Miungu watatu.

259 Hapo ndipo hamtaweza kamwe...Injili hii haitaenda kamwe kwa Wayahudi...Jambo ambalo, nilimtabiria asubuhi ya juzijuzi mmishenari wa Kiyahudi pale. Hutaweza kamwe kumpeleka Mungu wa utatu kwa Myahudi. Hutaweza kufanya jambo hilo kamwe. Ambapo, sivyo alivyo; yeye ana akili bora kuliko hiyo. Mnaona, yeye anajua zaidi juu ya Biblia kuliko jambo hilo. Bali Yeye kamwe si Mungu wa utatu, kwa— kwa Myahudi. Kama utamwacha ajue ni Yehova yeye yule, yeye atalipokea sasa hivi. Hakika! Hivyo ndivyo ilivyo, mnaona.

260 Nami ninaamini yote haya. Kama alivyosema Yusufu, "Ndugu, msijikasirikie, kwa maana Mungu amefanya jambo hili," mnaona. Kwa hiyo, kwa kuwa hilo jambo lilipaswa kungoja hata wakati huu, ni hayo tu, kwa maana wakati wetu wa Kimataifa uko karibu kwisha. Naam, ninaamini jambo hilo kwa moyo wetu wote. Kwa hiyo mnaona, ndugu zangu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninajaribu kufikia jambo fulani, ya kwamba, kundi hili la watu, la watu ambao wana ubatizo wa Roho Mtakatifu.

261 Kundi la Aimee McPherson, huyo mwanamke alifanya nini? Alikuwa wa Umoja kwanza, naamini; kisha akatoka akawa wa Assembly; halafu akatoka akajiundia madhehebu mengine; hapa si muda mrefu uliopita, akajiweka katika kundi dogo, kitu kidogo.

262 Nilikuwa nimeketi kwenye mkutano wa O. L. Jaggers. Naam, sote tunamjua. O. L. Jaggers. Baba ya—yake alisaidia kuanzisha Halmashauri Kuu ya Assemblies of God. Basi, O. L. ni mtu mashuhuri. Yeye ni mhubiri mashuhuri. Nilimwambia si muda mrefu uliopita, nikasema, "Ndugu Jaggers, kama ningaliweza kuhubiri kama unavyohubiri, kamwe nisingalifanya ibada ya kuponya." Bali yeye alikuwa na damu hiyo yote na divai, na kadhalika, wakati alipoanza kwanza kule.

263 Samahani, iwapo ninawaudhi, ndugu, juu ya jambo hilo. Mimi—mimi . . . Hilo ni sawa. Mungu anaweza kuifanya damu itoke, divai itoke, ama mafuta yatoke, cho chote anachotaka, bali jambo hilo haliondoi dhambi. La, bwana. La, bwana. La, hasha. “Damu ya Yesu Kristo haitapoteza nguvu Zake kamwe, mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa litakapookolewa, lisitende dhambi tena.”

264 Nilisema, “Ndugu Jaggers?” Nikamchukua; nikampigia simu. Nami nilikuwa pamoja na Wafanyi Biashara Wakristo. Nikasema, nikasema, “Ndugu O.L?”

265 Akasema, “Uko wapi basi?” Nilikuwa kwenye hoteli ya bei rahisi nje kule. Naye akasema, “Unataka kuniambia wao walikuweka huku nje?”

266 Nikasema, “Hivyo ndivyo nilivyotaka. Nilipokuja kwenu,” nikasema, “mlifanya nini? Mliniweka kule kwenye Hoteli ya Startler, nami ilinibidi kusimama pembeni. Wao waliniketisha mezani; sikujua nitumie kisu gani, wala cho chote kile. Nami siku-. . . Nikashuka nikaenda kule bila koti, nao walitaka kunifukuza.” Ndipo nikasema, “Si—sijui jinsi ya kujishughulikia.”

Akasema, “Mimi nitakupeleka kule, kama wao ni maskini sana wasiweze kufanya hivyo.”

267 Nikasema, “La, bwana.” Nikasema, “Kile ninachotaka kufanya ni kula nyama choma pamoja nawe, kama utaigharimia.”

Akasema, “Sawa.”

268 Kwa hiyo tukatoka tukaenda mahali fulani, tukaketi. Ndipo nikasema, “Ndugu Jaggers, bila shaka naheshimu nini hii yako . . . ”

269 Naye ni rafiki msiri wangu, ndugu wa thamani. Nami ni—nilikuwa na kitini chake kidogo, naye . . . ambapo alikuwa na yule mwanamke ambaye ndiyo kwanza aje huku kutoka nchi za ng’ambo, aliyekuwa na damu mikononi mwake, na kadhalika. Kwa hiyo nilikuwa nacho humu ndani. Nilitaka tu yeye akikane mara moja, halafu nilikuwa nimelipata moja kwa moja katika gazeti—katika gazeti lake, mwajua.

270 Nikasema, “Nimeona mahali unapoelekea moja kwa moja, ukiwa, utakuwa na ufufuo mkuu, ulianza.” Maana, Wafanyi Biashara walikuwa wamenipeleka kule, bila shaka.

271 Inaonekana kama kwamba watu wangejua. Kama Roho Mtakatifu anaweza kufunua jukwaani, hivi hawezi kuniambia yale yanayotendeka mahali mbalimbali, ndugu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

272 Ninaweza kuwaambia neno kwa neno, na kuwathibitishia kwa Ndugu Carlson, na ndugu huyu *hapa*. Niliketi mkutanoni, jana, na kuwaambia ndugu hawa kile kitakachotukia hapa

asubuhi hii. [Ndugu fulani anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Hiyo ni kweli. Kweli kabisa. ["Amina."] Mnaona? Kwa maana, Roho Mtakatifu aliniamsha, akasema, "Simama karibu na dirisha." Nikaangalia, dirishani, Naye akanionyesha jambo *hili* kabisa. Nikasema, "Sasa, ndugu . . ." [Ndugu fulani anasema, "Hiyo ni kweli."] Niliwaonyesha jambo hili, kweli kabisa. Pale! Mnaona?

Mbona, wao wanapaswa kujua jambo hilo.

273 Hapa si muda mrefu uliopita, mtu fulani aliinuka, hapa Chatauqua, akasema, "Ndugu Branham ni nabii." Sidai kuwa nabii. Mnaona? Bali yeye alisema, "Ndugu Branham ni nabii wakati yuko chini ya Roho wa upambanuzi, lakini, akasema, "loo, Mafundisho yake ni sumu. Jihadharini nayo." Nikawazia, hivi mtu mwenye elimu, angesema jambo kama hilo.

274 Maana ya *nabii* ni nini? "Mfasiri wa Kiungu wa Neno." "Neno la Bwana lilimjia nabii," mnaona. Lakini, hilo tu, hilo si hoja.

275 Lakini, hata hivyo, Ndugu Jaggers. Nami nikasema, akasema, loo . . . nikasema, "Niliona habari za mwanamke yule aliye na damu mikononi mwake."

276 "Loo," akasema, "Ndugu Branham, hilo ndilo tukio la ajabu sana ulilopata kuona!"

277 Nikasema, "Ndugu Jaggers, nakupenda. Kwanza, nataka uuweke mkono wangu juu ya wako. Hebu tuseme sisi ni ndugu."

Akasema, "Hakika. Kuna nini?"

278 Nikasema, "Wewe ni mmoja wa wahubiri hodari sana nijuao. Jinsi—jinsi wewe ulivyo chombo cha Mungu!"

279 Akasema, "Asante, Ndugu Branham. U mnyenyekevu sana."

280 Nikasema, "Sisemi jambo hilo kusudi niwe mnyenyekevu. Ninasema jambo hilo kwa sababu ninaamini wewe ni mtumishi wa Mungu." Lakini nikasema, "Ndugu Jaggers, usipokuwa . . . Una—Unatoka nje sana; huna ya kupimia mizani yale unayonena. Unaweka msingi . . ."

281 Basi hii ndiyo shida ya wengi wenu ninyi Assemblies of God, na watu wengine, juu ya hizi ibada za kuponya. Siwalaumu. Kuna nyingi mno zinazoitwa . . . Naye Tommy, hapa, ni ndugu mzuri, nasi tunajua jinsi anavyosimama imara. Bali kuna mengi sana nchini leo chini ya jina la kuponya Kiungu, si ajabu hamtaki kudhamini mkutano humu jijini. Wao wanakuja na kuwanyonya watu, kisha wanaondoka. Nao wanapata nini? Hawawapi watu zaidi kidogo kuliko mnavyofanya jukwaani, kwenye mimbara yenu wenyewe. Nanyi mko sahihi, ndugu. Ninawaambia, mko sahihi. Lakini ni kama tu . . .

282 Nilikuwa nikisoma historia ya Martin Luther. Inasemwa, "Siri si ya kwamba Martin Luther aliweza kulipinga kanisa

Katoliki na kufaulu." Mmeisoma hiyo historia yake. "Lakini kwamba Martin Luther angeweza kukiinua kichwa chake juu ya ushupavu wote wa dini ulioufuata ufufuo wake, hiyo ndiyo ilikuwa siri."

283 Basi wakati mambo ya ajabu yamekwisha, wasiotahiriwa walifuata, kama tu ilivyokuwa kule Misri. Na daima jambo hilo limesababisha shida kutokea nchini. Tunajua jambo hilo, tunapoenda huko. Ambapo, wao walimwinua Kora, hata ikambidi Mungu kuliangamiza. Lakini, ndugu, mimi siwalaumu.

284 Ndugu Jaggers aliketi pale akajaribu kuniambia ya kwamba huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu aliyekuwa akifanya hivyo. Kisha kasema . . . Nami niliiliona, kwenye gazeti lake mwenyewe . . . Nikasema, "Ndugu Jaggers, sasa," nikasema, "mimi ni mwanafunzi wa darasa la saba. Nawe ni Daktari wa Kiungu, na umesomea uwakili. Ulikuzwa katika kanisa safi, lenye ustahifu, Assemblies of God. Baba yako alisaidia kuanzisha imani hiyo. Nawe ukajiondoa, hiyo ni juu yako." Lakini, nikasema, "Hiyo ni juu ya mtu ye yote, anayetaka kufanya jambo hilo. Mimi siweki mpaka wo wote hapo. Bali inapofikia mahali ambapo chombo kama wewe, unayeweza kuwavuta maelfu ya watu kwa Kristo, ungejenga huduma yako juu ya mwamsho." Nikasema, "Ndugu Jaggers, ukijenga mnara kama *huo*, kama huna timazi, utaanguka baada ya kitambo kidogo. Nawe huna budi kuwa na Maandiko kwa ajili ya jambo unalonena."

Akasema, "Kuna Maandiko."

Nikasema, "Yatoe!"

285 Akasema, "Vema, Ndugu Branham," kasema, "Huyo anayefanya jambo hilo ni Roho Mtakatifu."

286 Nikasema, "Nionyeshe, Maandiko, ambapo yalisema Roho Mtakatifu alifanya damu itoke kutoka kwa mtu fulani, na kadhalika, namna hiyo. Nionyeshe tu; mafuta yakiwatoka. Ulisema, 'Mafuta hayo yalikuwa kwa ajili ya kuponya Kiungu.' Kisha ukasema, 'Damu ya mwanamke huyo ingekuwa kwa ajili ya wokovu wa mataifa.'" Nikasema, "Kama hiyo ni kweli, basi ilikuwaje kwa Damu ya Yesu Kristo! Hilo linaiondoa. Na cho chote ambacho kinaipinga Hiyo, ni mpinga. Kinaipinga." Nikasema, "Inakuwa fundisho la mpinga Kristo."

"Loo," akasema, "Ndugu Branham, utajua siku moja."

287 Nikasema, "Ninatumaini sitajua jinsi hiyo. Sasa, ndugu," nikasema, "ninakupenda, nawe ni ndugu yangu." Kisha nikasema, "Ndugu Jaggers, utaenda kando, baada ya muda kidogo, ambapo usingeweza kurudi. Rudi kanisani mwako, na urudi na ukadumu na Injili!" Kisha nikasema, "Usijenge juu ya miamsho." Nikasema, "Ile . . . "

288 Sasa yeye, yeye anawabatiza katika Uzima wa Milele, mwajua, "Kila unapobatizwa, unarudi ukawa kijana mwanamke ama mwanamume. Sasa hilo lita-. . .Hutakufa (kamwe)." Kwa hiyo, jambo hilo, hilo, sasa amefikia mwisho wa njia sasa hivi; na hivyo vidonge vya "vitamini kutoka Bahari ya Chumvi." Mnaona? Lakini hivyo ndivyo ilivyo, ndugu, yeye alianza na miamsho hiyo midogo.

289 Nanyi watu hapa mlio na makanisa haya, mnaachilia kitu kama hicho kije mjini, nanyi, mwajua, Ibilisi ni mjanja, naye a—anaruka ndani ya vitu hivyo namna hiyo. Anafanya fujo kwake. Anawafanya watu wafikie hatua ya mwisho, naye anasababisha mchafuko kanisani, na kadhalika. Bali sivyo ilivyo.

290 Naam, hapa. Haidhuru u sahihi jinsi gani, hili hapa jambo moja ambalo tunashidwa na kukosa, ndugu zangu. Sasa ninafunga, kwa kusema jambo hili. Haidhuru mimi ni sahihi jinsi gani, jinsi nilivyo wa kimaandiko, na jinsi ninavyoijua Biblia ya Mungu; iwapo sina Roho wa Mungu, wa upendo, moyoni mwangu, kwa ajili ya jamii nzima ya binadamu na kadhalika, basi mimi kwanza nimekosea.

291 Naam, Paulo alisema, katika Wakorintho wa Kwanza 13, "Nijapokuwa na maarifa, mnaona, na kufahamu siri zote za Mungu, manaona; chini ya yote, kusimama; wala sina upendo, si kitu mimi. Nijaponena kwa lugha za wanadamu na za malaika," hizo ni zile unazozungumza na Mungu, na daima zile zinazoweza kufasiriwa. "Nijaponena kwa lugha, lugha halisi za wanadamu na za malaika, wala sina upendo, upendo, hainifai kitu." Kwa hiyo kama ninajua siri zote za Mungu, na ninaweza kuzifunua na—na kuzifanya zote ziungane pamoja, nami sina upendo, inafaa nini? Na wakati mimi . . .

292 Yesu alisema, "Kwa jambo hili watu wote watatambua ya kwamba ninyi mmekuwa wanafunzi Wangu, mkiwa . . ." wakati wa Assemblies wanawapenda wa Umoja, na wa Umoja wanawapenda wa Assemblies, "mkipendana, ninyi kwa ninyi," mwe sahihi msiwe sahihi. Na mradi tu nia ni baya, kusudi ni baya, hasa, basi kwanza ninyi mmekosea. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona, "Nijaponeana kwa lugha ya wanadamu na ya malaika, wala sina upendo, bado mimi si kitu." Kwa maana, Mungu ni upendo. Tunajua jambo hilo.

293 Nami ninaamini katika kunena kwa lugha. Naam, mtu fulani alisema, "Ndugu Branham haamini katika ushuhuda wa kwanza." Ningetaka kulifanya hilo dhahiri kwenu sasa. Mnaona? Ningetaka kuwaambia.

294 Ninaamini ya kwamba mtu anapompokea Kristo, anapokea sehemu ya Roho Mtakatifu. Maana, Yesu alisema, katika Mathayo sura ya—ya 12, ya sura ya 5 na aya ya ishirini . . . aya ya 24, Yeye alisema. La, naamini ni Yohana Mtakatifu 5:24. Alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye

aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele." Naam, kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. "Naye hataingia hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

295 Naam, ninaamini ya kwamba hakuna mtu anayeweza kujiita mwenyewe; Mungu hana budi kumwita. Na iwapo Mungu kweli alimwita. . .Na kuna watu wengi sana, tunajua, ndugu, ambao wamechochewa na wanafikiri ya kwamba Mungu amewaita, bali maisha yao karibuni. . .yata-, yatakudhihirisha. Bali kama Mungu anakuita, mbona, wewe utakuwa pale, nawe utakaa pale, unaona, fahamu. Na kama. . . Naam, hilo si fundisho la Kibatisti. Mwajua jambo hilo, mnaona.

296 Lakini, bila shaka siamini katika kupeana mikono na kuwa na usalama wa Milele, na upuzi huo wote. Si—siamini katika jambo hilo, hata kidogo. Kama wao wanataka kuamini jambo hilo, vema, hilo ni sawa. Ningali ninasema wao ni ndugu zangu.

297 Asubuhi hii, kama ningeomba kipande cha sambusa, (ambapo ni karibu wakati wa chakula cha mchana), huenda nikapenda ya tunda jekundu, nawe huenda ukala ya tofaa, bali sote tunakula sambusa. Mnaona? Kwa hiyo haileti. . .yo yote, mradi tu tunakula sambusa.

298 Hivyo ndivyo tunavyoamini. Kama unataka kuwa wa Umoja, kuwa wa Umoja; kama unataka kuwa wa Assembly of God, kuwa wa Assembly of God. Ukitaka kuwa cho chote kile, Batisti, Presbiteri, kuwa Mkristo humo. Unaona?

299 Basi—basi jitafutie mwenyewe, bali msizozane mmoja kwa mwingine. Kwa sababu, vitu hivi vidogo, vyote vinaambatana pamoja. Hiyo ni kweli. Vyote vinaambatana pamoja na kufikia mahali hapo pamoja.

300 Na—na haidhuru tufanye nini, ni miujiza mingapi tunayoweza kufanya, ni milima mingapi tunayoweza kuhamisha, ama cho chote kile; mpaka tutakapofikia mahali ambapo tunapendana, si kujifanya kuamini, bali tunapendana sisi kwa sisi. Wakati tunapompenda kila ndugu, haidhuru yeye ni mshirika wa kanisa lipi, tunampenda; si kujifanya tu tunampenda, kwa sababu tunajua ni wazo la kidini, ni, "Tunapaswa kufanya jambo hilo." Bali, kwa sababu tunafanya jambo hilo, tunapendana; basi, uvumilivu, kuvumiliana sisi kwa sisi.

301 Nami naamini, katika Wakolosai 3, yapata 9, mahali fulani mle. . .Huenda mimi, si—si-. . .Huenda nimekosea katika Maandiko, bali yalisema haya. Baada ya sisi kuwa Wakristo, hatupaswi kuwa na kijicho. Mnaona? Hatuwezi kuwa na imani wakati tunapojaribu kupendeleana na kuheshimiana. Mnaona, hatuwezi kufanya hivyo; hatuwezi kuwa na imani. Hatuna budi kumheshimu Mungu, mnaona, kumheshimu Yeye. Kuwaamini ndugu zangu, bila shaka, ni upendo; bali heshima na staha ni za Mungu! Kuhusu nini hii. . .Lakini muwe na imani na

kuaminiana ninyi kwa ninyi. "Wala msiambiane uongo ninyi kwa ninyi." Mnaona? "msiambiane uongo ninyi kwa ninyi." Kama nikikwambia asubuhi ya leo, "Nawapenda," sina budi kumaanisha jambo hilo. Kama silimaanishi, mimi ni mnafiki. Hiyo ni kweli hasa.

302 Naam, ndugu, kwa njia hii . . . Naam, Ndugu Tommy, natumaini sijawacheleweshа sana hapa. Mimi . . . Ndugu Tommy ana jambo la kusema kwa muda kidogo tu. Lakini huenda nikasema jambo hili, ninapokuja katikati yenu . . .

303 Ninaamini jambo hili. Ninaamini ya kwamba Mungu Baba yetu alimtia uvuli bikira aliyeitwa Mariamu, na kuumba ndani yake chembechembe ya Damu ambayo ilimzaa Yesu Kristo, ambaye alikuwa Mwana wa Mungu, maskani ambamo Mungu alijificha Mwenyewe, katika mwili, akajidhihirisha Mwenyewe miongoni mwetu. "Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Ninaamini ya kwamba chembechembe hiyo ya Damu ilivunjwa pale Kalvari, kwa ajili la ondoleo la dhambi zetu. Ndipo Roho akamtoka Yeye na kurudi juu ya Kanisa, kwa sababu, yule Kristo, Roho Mtakatifu; Kristo, yule Logos, alikuwa ndani yetu sasa, Roho Mtakatifu, kwa ubatizo. Akitufanya . . . Kristo alijitenga Mwenyewe, akitoa Uhai Wake kwa ajili ya kila mmoja wetu, kusudi sisi, kama kundi la watu, tupate kuwa Kanisa la Mungu. Na si muda mrefu uliopita . . .

304 Nilizoea kupanda farasi. Mnajua jambo hilo. Baba yangu alikuwa mpanda farasi, mwenye shabaha sana. Nilizoea kupanda farasi. Tuliwachunga nini—nini hii . . . katika Bonde la Arapaho, ama namaanisha Mto wa Troublesome, ng'ambo ya Safu ya Arapahoe. Shirika la Hereford linawalisha kwenye bonde hilo. Na kwenye bonde hilo, hao watu wa ranchi, wana—wana nyasi nyingi sana hata wanazoweza kukuza. Na wakati ranchi moja itatoa kiasi cha tani moja ya majani yaliyokaushwa, unaweza kumchunga ng'ombe kwenye hayo ma—malisho, kule chini ya Estes Park kule, pia unaweza kumchunga ng'ombe kwenye hayo ma- . . . Sehemu yangu nzuri sana ya kuwindia kule juu. Nami nimewachunga ng'ombe kule mwaka mmoja. Ningali ninaenda bado, kwenye msimu wa Kupukutika Majani na Mwishoni mwa Mwaka, ninapokuwa likizoni na nikiwapo na uwezo, nami napanda farasi kuwakusanya ng'ombe, ili kwamba tu niwe kule juu, kwa maana ninapenda kupanda farasi. Na kila mahali juu chini kwenye ile ran- . . . bonde lile, kuna kundi la wanaranchi walio na haki ya mahali hapa, kuwalisha ng'ombe wao. Na kwenye majira ya Kupukutika Majani, mara nyingi, nimewasaidia kuwakusanya ng'ombe na kuwapeleka kule.

305 Na kuna ua la kuwazuia, ambapo hawawezi kurudi kwenye mali ya mtu, wanaposhuka kwenye ile safu ya milima. Mpaka . . . Naye msimamizi anasimama pale na kuwahesabu hao ng'ombe anapoingia, wanapoingia. Nami nimeketi, siku nyingi, saa

baada ya saa; nikiliangalia kundi la Bw. Grime likiingia, alikuwa na Mkuo wenye alama ya Almasi, wetu walikuwa na alama ya Bata Mzinga; nao walikuwa na alama ya—ya Kiti chenye miguu mitatu chini yetu; na alama ya Jefferies, na kadhalika. Kisha, nilipouweka mguu wangu, kama wengi wenu mjuavyo, kwenye kichwa cha matandiko, na kuketi pale na kumwangalia yule msimamizi alipokuwa amesimama pale, akiwahesabu ng'ombe hawa.

306 Niliona jambo moja. Hakuijali sana alama iliyokuwa juu yake. Bali kuna kitu kimoja alichochunguza sana, hicho kilikuwa kipande kilichoonyesha ukoo wake. Ilimbidi awe wa ukoo halisi wa Hereford la sivyo asingeenda nyuma ya ua ule, bali alama yake haikufaa sana.

307 Nami nafikiri hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye ile Hukumu. Yeye hataangalia alama zetu, bali ataangalia kile kipande cha kuonyesha Ukoo.

308 Nimefanya makosa yangu, ndugu, na nimefanya mambo mengi sana ambayo ni mabaya. Na kama wakati wo wote njiani nimeleta, ama mmesikia kitu fulani ambacho huenda nimekitaja ama kukisema, ambacho kwa namna fulani kinaudhi, ama kama nilisema jambo fulani asubuhi ya leo ambalo liliudhi, ninawaomba, kama ndugu Mkristo ama dada, mnisamehe. Sikusudii kufanya hivyo. Nimewatolea tu yaliyo moyoni mwangu, ili kwamba tupate kujua.

309 Kama kuna ubatizo wo wote utakaofanywa, ninyi ndugu ufanyeni, wenyewe, mnaona. Hiyo, mimi—mimi sifanyi jambo hilo. Kama ningalifanya hivyo, hivyo ndivyo nitakavyombatiza, wa namna hiyo. Na mmoja wenu anayeweza kuukubali, mnaona. Kwa hiyo, unaweza kumchukua mtu, wanabatizwa katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, na wanabatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo, pia. Kwa hiyo kama nikipata kumbatiza mtu. . . bali sijafanya hivyo bado. Ninabatiza tu katika kanisa langu mwenyewe, na hiyo ni hao watu tu kule. Na hivyo ndivyo watu kanisani mwangu wanavyobatizwa. Na kama ukiangalia kule nyuma, huo ni utaratibu wa kale wa Kimishenari, utaratibu wa kale wa Batisti ya Kimishenari. Na sasa iwapo. . . Hivyo ndivyo ilivyo.

310 Ninaamini katika kuponya Kiungu. Ninaamini katika Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ninaamini katika—katika Roho Mtakatifu kunena kwa lugha. Ninaamini katika kila kipawa ambacho Mungu alilipa Kanisa Lake. Ninaviunga mkono, asilimia mia moja. Lakini ninaamini . . .

311 Siungi mkono baadhi ya kuponya huku kwa hali ya juu sana tuliko nako siku hizi. Ningetaka tu kutoa tamshi hapa. Siku moja kulikuweko na ndugu fulani . . . wala si Ndugu yangu mpendwa Tommy Hicks, ambaye ninamchukua kama mtumishi halisi wa Kristo. Kulikuwa na mtu mwingine katika nchi nyingine, na

katika nchi hii kulikuwa na. . . Yeye alikuwa tu, kila wakati, "Mponya wa hali ya juu wa Mungu; mponya wa hali ya juu wa Mungu," mwajua, namna hiyo.

312 Nami nikapokea barua baada ya huyo mtu ku-. . . kutoka kanisa la Kiluteri. Na katibu wangu hapa anajua tunayo kwenye faili. Nisingelitaja jina la huyo mtu, kwa maana si tabia ya Kikristo. Ingawa, sikubaliani na mawazo ya huyo mtu, bali hilo ni sawa kabisa. Ninampenda. Yeye ni ndugu yangu.

313 Lakini imefikia mahali ambapo hawana budi kuwa tu na namna fulani ya mwamsho, ama kuuchochea, ama kitu fulani ama kingine kama hicho, mnaona. Basi, jambo hilo, jambo hilo si zuri, unaona. Ndugu. . . "Mazoezi ya mwili yana faida kidogo sana."

314 Na kwa hiyo Mluteri huyu akamwandikia mhudumu huyu ba—ba—barua. Akasema, "Ninyi wainjilisti wa Kimarekani mnaokuja hapa," kasema, "pamoja na kuponya kwenu kwa hali ya juu sana kwa kila mtu!"

315 Basi sasa hili linasikika kama shada dogo la maua kwa ajili yangu, bali Mungu anajua silikusudii hivyo. "Lakini," akasema, "wakati maskini Deborah Stadsklev alipokufa, yule mtoto mchanga, na mama yule alikuwa amesimama pale siku ile huko India-. . . California, ambapo yule mtoto mchanga alikuwa amekufa, na akawa baridi. Na kuona . . . wakamweka mtoto huyo mchanga mikononi mwa Ndugu Branham, huku amesimama pale na kumwombea. Ndipo huyo mtoto akaanza kulia kwa sauti kuu na kutupatupa miguu; kisha akamrudisha kwa yule mama."

316 Yeye pia alijua juu ya kisa kile cha Mexico. Ambacho, tunaweza kuchukua taarifa hii ya Wafanyi Biashara wa Injili Yote. Huna budi kuwa na kitu fulani kilichoandikwa na daktari. Wakati mtoto yule mchanga wa Kimexico alipokufa ile asubuhi, kwenye saa tatu, na hii ilikuwa saa tano usiku. Daktari aliandika taarifa yake. Ndugu Espinoza, ambaye wengi wenu enyi ndugu wa Assemblies of God mnamjua, ilikuwa ndiye aliyechukua taarifa hiyo kutoka kwa daktari, ya kwamba amekufa.

317 Ndipo niliona ono huko nje juu ya umati wa watu; wakati Wakatoliki elfu ishirini walipomjia Kristo, katika Jiji la Mexico. Nikasema, "Usichukue tu hilo. Sijui, mtoto huyo mchanga. . . Ndiyo kwanza nione ono hapa nje."

318 Naye Billy alikuwa pale, akijaribu, pamoja na mabawabu wengine thelathini ama arobaini, wasingeweza kumzuia maskini mwanamke yule asiingie kwenye mstari wa maombi, pamoja na mtoto yule mchanga. Angekimbia akapita katikati ya miguu yao, na kadhalika. Kwa hiyo, hatimaye, nikamtuma Jack Moore kule. Nikasema, "Nenda, ukamwombee."

319 Nikaangalia kule nje, nami nikamwona maskini mtoto mchanga wa Kimexico akitabasamu. Nikasema, "Ngoja kidogo. Mlete hapa." Mnaona? Nami nilipouweka mkono wangu kwenye

blanketi ile...Mvua ilinyesha, siku nzima. Nao walikuwa wamesimama pale tangu asubuhi ile na mapema, na hii ilikuwa yapata saa tano usiku huo. Basi nikaiweka mikono yangu juu ya huyo mtoto mchanga. Akaanza kutupatupa miguu na kulia. Nao wakaanza kupiga mayowe.

320 Kwa hiyo, basi wakamchukua wakapate taarifa. Wakaenda kwa yule daktari, naye daktari akasema, "Nilimtangaza huyu mtoto mchanga kwamba amekufa, asubuhi ya leo saa tatu. Alikufa kwa niumonia." Mnaona? Na kwa hiyo basi mambo hayo ni—ni—ni kweli. Hizo ni taarifa. Hazina budi kuwa ni kweli.

321 Tunapaswa kuwa waaminifu na wa kweli kuhusu cho chote. Usilifanye nini hii yo yote...Acha tu liwe jinsi lilivyo. Hebu... Mungu hahitaji usaidizi wo wote juu ya cho chote kile. Mnaona, Yeye—Yeye—Yeye ni Mungu.

322 Kwa hiyo akasema jambo hili sasa, "Lakini wakati mama huyu alipompigia simu Ndugu Branham kule Marekani, akimlilia kwenye simu, 'Njoo ukamfufue mtoto wangu mchanga!' Na serikali ya Marekani..."

323 Mumewe ni kasisi Jeshini. Nanyi nyote mnamjua Julius, wengi wenu wanamjua; aliandika kile kitabu changu, *Nabii Aizuru Afrika*.

324 Basi maskini mama huyo wa Kinorway, akilia, kwa sauti yake yote, alisema, "Ndugu Branham, nilikuwa nimesimama pale wakati mtoto huyo mchanga alipofufuka!" Kasema, "Tunakuamini wewe kwamba ni mtumishi wa...wa Kristo." Kasema, "Njoo, ukaweke mikono yako juu ya mtoto wangu mchanga, naye ataishi." Alikuwa amekufa katika dakika moja ama mbili, kwa niumonia; alikuwa mgonjwa kwa yapata masaa manne, ama matano.

325 Na watu hawa walikuwa wamezunguka pale, wakipiga mayowe na kupaza sauti, na kurukaruka, wakisema, "Mungu atamfufua! Mungu atamfufua!" Kisha akasema...

326 Kwa jambo hilo, nini hii ya Marekani...ama, si Shirika la Marekani la Ndege. Jeshi la Marekani lilikuwa linirushe kule kwa ndege, na kunirudisha, katika siku moja. Mnaona?

327 Nami nikasema, "Kabla ya mimi kuja, hebu nitafute mapenzi ya Bwana." Kwa hiyo nikaomba, siku mbili. Naye yule daktari alikuwa mwema sana kumwacha yule mtoto alale pale.

328 Ndipo, asubuhi moja, niliamka nikaanza kutembea kule jikoni. Nikaangalia; ilikuwa ni Nuru tu, imesimama kule, pale, yapata ukubwa wa ile taa pale, inazungukazunguka, kasema, "Usimguse huyo. Usikemee jambo hilo. Huo ni mkono wa Bwana."

329 Nikakimbia nikarudi na kulipigia taifa simu, nikapiga simu nikasema, "Si—siwezi kuja."

330 Basi mhudumu huyu wa Kiluteri akasema, "Kwa nini msingojee mpaka mpate uamuzi dhahiri kutoka kwa Mungu, kama alivyofanya Ndugu Branham, ndipo mtajua mnalozungumzia!"

331 Naam, hivyo ndivyo ilivyo, ndugu, iwapo hatutaamua mambo haraka; na kungoja, na kupata maamuzi dhahiri, na halisi kutoka kwa Mungu.

332 Na vituo hivi vyote hapa, vya kuponya ambavyo havijui kitu juu ya Mungu. Ninaamini ya kwamba kuponya Kiungu kumewekwa juu ya kanuni, ya kwamba unapaswa kuja kwa Mungu, kwanza, na kumpa Yeye moyo wako, na kusafisha maisha yenu katika Damu ya Yesu Kristo, ndipo Mungu atakutendea kazi na kukuponya. Kama tu ndugu huyu alivyosema, juu ya maskini yule mwanamke aliyemwombea kule chini, mtakatifu wa Mungu, mnaona.

333 Katika maisha yangu, nilifanya makosa mengi. Nimefanya mambo mengi mabaya. Labda, kama nikiishi muda mrefu zaidi, nitafanya mengi zaidi. Labda mengine yatakuwa vikwazo njiani mwenu. Natumaini ya kwamba mtanisamehe.

334 Nilikuwa nikisoma juu ya Ibrahimu, jinsi ambavyo vipingamizi alivyokuwa navyo. Jinsi ambavyo yeye, jamani, mambo aliyofanya; alimshuku Mungu; kisha akasema uongo juu ya mkewe; na kila kitu. Bali wakati maelezo yake ya Kiungu yalipoandikwa katika Warumi 4, hayakutaja makosa yake, bali yalisema, "Ibrahimu hakusitasita" katika kutokuamini . . . katika Mungu, "bali alikuwa mwenye nguvu." Makosa yake yote yalisahauliwa kabisa, wakati yale maelezo ya Kiungu ya maisha yake yalipoandikwa. Vipingamizi vyake hata havikutajwa. Makosa yake hayakutajwa.

335 Basi, ndugu, natumaini, ya kwamba wakati maelezo yangu yatakaposomwa kwenye Siku ile, ya kwamba Yeye atayafutilia mbali yangu, pia, wala hatayawazia. Natumaini mtafanya hivyo, pia. Mungu awabariki.

336 [Ndugu Tommy Hicks anatoa maelezo, kisha anaomba. Kusanyiko linamsifu Mungu, kisha linaimba *Nampenda*. Ndugu wanakumbatiana mmoja kwa mwingine, nao dada wanakumbatiana mmoja kwa mwingine. Baada ya dakika nane, Ndugu Branham anarudi kwenye maikrofoni—Mh.]

337 Kama ningeweza kuona jambo hili likitendeka kila mahali ulimwenguni mwote, ningesema, "Bwana, mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani!"

Kuelezewa Kwa Uungu SWA61-0425B
(The Godhead Explained)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumanne kifunguakinywa, Aprili 25, 1961, katika Holiday Inn kule Chicago, Illinois, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2004 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org